Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA ISHIRINI

**Kikao cha Pili - Tarehe 8 Juni, 2005**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UBINAFSISHAJI):-**

Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2004 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2005/2006.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:-**

Taarifa ya Sera za Fedha kwa kipindi cha Mwaka 2004/2005 na Mwelekeo wa Sera za Fedha kwa Mwaka 2005/2006.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 11

### Ugawaji wa Wilaya ya Mbozi

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya ya Mbozi ni kubwa sana na ina idadi ya watu 515,000 au zaidi wakati Wilaya nyingine zina watu kati ya 100,000 na 300,000 tu na kwamba Wilaya hiyo inatimiza vigezo vyote vya kuweza kugawanywa:-

(a) Je, kuna mpango wowote wa kuigawa Wilaya hiyo ili kuweka uwiano mzuri na wa haki wa Maendeleo kwa wananchi wetu?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kulingana na wingi wa watu hao ingefaa pawepo na Majimbo walau matatu (3) au zaidi ili haki ya uwakilishi ionekane kuliko ilivyo sasa kwa kuwepo Majimbo mawili tu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mbunge wa Mbozi Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge lako Tukufu, tarehe 11.11.2003, Ofisi yangu ilijibu swali Na.74 lililoulizwa na Mheshimiwa Eliachim Simpasa linalofanana na swali hili. Katika majibu yangu nilieleza bayana kuwa utaratibu wa kuunda au kugawa maeneo ya kiutawala hapa nchini unatawaliwa na Sheria za Serikali za Mitaa Na.7 (Mamlaka za Wilaya) na Na.8 (Mamlaka za Miji) za mwaka 1982 na Sheria ya Taratibu za Uanzishaji wa Mikoa na Wilaya Na.12 ya Mwaka 1994. Sambamba na sheria hizi, vigezo muhimu vinavyotumika kuanzisha Wilaya mpya ni pamoja na:-

- Ukubwa wa eneo lenye kilomita za mramba zisizopungua 5,000;
- Idadi ya Tarafa zisizopungua 5;
- Idadi ya Kata zisizopongua 15;
- Idadi ya vijiji visivyopungua 50;
- Idadi ya watu wasiopungua 100,000;
- Eneo lenye jiografia ambayo inazuia huduma kuwafikia wananchi kwa urahisi kama vile milima, mito, misitu mikubwa, visiwa n.k.

Mheshimiwa Spika, maana halisi ya vigezo hivi ni kwamba eneo linalokidhi vigezo hivi ni eneo linaloweza kusimamiwa na Mkuu wa Wilaya kwa ufanisi zaidi na hivyo kuleta maendeleo ya haraka kwa wananchi. Kwa maneno mengine kama tukizingatia kigezo cha idadi ya watu Tanzania Bara ambayo inakadiriwa kuwa na watu 33,584,605 inapaswa kuwa na Wilaya zipatazo 376 na tukitumia kigezo cha ukubwa wa eneo Tanzania Bara lenye eneo la *Sq.kms.881,289* inapaswa kuwa na Wilaya zipatazo 176.

Kulingana na hali halisi ilivyo hivi sasa, Wilaya nyingi hapa nchini zinastahili kugawanywa katika maeneo mawili au zaidi. Kwa kulitambua hili, Ofisi yangu iliamua kufanya uchambuzi wa kina katika Mikoa na Wilaya ili kuwa na picha kamili ya mwelekeo wa mahitaji ya kugawa maeneo mapya ya utawala badala ya kungoja maombi. Uchambuzi huu ulibaini kuwa kwa kuzingatia vigezo vya ukubwa wa eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 5,000 na idadi ya watu 200,000-350,000 ili nchi yetu itawalike kwa urahisi kidogo Wilaya mpya zipatazo 24 zinatakiwa kugawanywa ikiwemo Wilaya ya Mbozi. Wilaya zingine ni pamoja na Mpanda, Kilosa, Bariadi, Mbinga na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ugawaji Wilaya unakadiriwa kuigharimu Serikali kiasi kikubwa cha fedha takriban shilingi bilioni moja kwa Wilaya. Kwa kuwa Ofisi yangu tayari imebainisha jambo hili, uwezo utakapopatikana utekelezaji wake utaanza awamu kwa awamu.

(c) Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mbozi kwa hivi sasa ina Majimbo mawili ya Uchaguzi ambayo ni Mbozi Mashariki na Mbozi Magharibi. Uongozi wa Wilaya ya Mbozi uliwasilisha hoja ya kutaka kugawa Majimbo ya Uchaguzi katika Mkutano wa Kamati ya Ushauri ya Mkoa wa Mbeya uliofanyika tarehe 6 Mei, 2004. Pamoja na mambo mengine yaliyojadiliwa agenda iliyohusu mapendekezo ya kugawa Majimbo ya Uchaguzi ilijadiliwa. Majimbo yaliyopendekezwa ni Vwawa, Igamba, Ndalambo na Bonde la Ufa. Maombi hayo hayakuweza kupitishwa na kikao hicho kwa sababu Serikali ilishatamka ya kwamba kwa kipindi cha 2000 - 2005 hakukuwa na uwezekano wa Serikali kuendelea kugawa Majimbo ya Uchaguzi ili kuwezesha zoezi la kuandaa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura lenye gharama kubwa kukamilishwa kwanza ipasavyo. Kwa hiyo, kwa kipindi hiki cha 2002-2005, kwa kweli Serikali haina mpango wowote wa kuigawa Wilaya hiyo katika Majimbo manne.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza, nashukuru sana kwa majibu mazuri tu ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyatoa hivi punde. Kwa kuwa viwango vyote alivyovitaja Mheshimiwa Naibu Waziri, sisi katika Wilaya yetu tumevuka na zaidi yaani kupita kiasi, sasa shida kubwa ni fedha au ni masuala mengine tu kwa sababu mwaka jana 2004 wamegawa Wilaya nyingine ndogo ndogo tu? *(Kicheko)*

Pili, katika ukubwa wa Majimbo yetu mimi na Mheshimiwa Halinga na baadhi ya Wabunge wamepita katika Tarafa moja tu ya Ndaramo walishangaa sana. Katika hali hiyo, Mbunge mmoja anapobebeshwa mzigo mkubwa namna hii wakati mwingine ana Kajimbo kadogo anaweza kupiga kengele tu wananchi wote wakaja kuna uhalali gani hapo, tunasaidiwaje sisi? *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, katika maelezo yangu ya msingi, nimebainisha wazi kabisa kwamba zoezi la awali limekwishafanyika kwa maana ya kujua tu kwamba ili Taifa letu litawalike kwa urahisi ni vitu gani tunaweza tukajaribu kuviangalia. Tumeshakamilisha zoezi hilo na ndio maana nimethubutu hata kusema Mbozi ni moja kati ya Wilaya zile ambazo ziko katika kipaumbele cha kwanza kutokana na ukubwa wake pamoja na Wilaya nyingine nilizozitaja.

Kwa hiyo, kwa kweli kwa sasa nadhani tatizo kubwa ni fedha. Lakini vile vile lazima zoezi hili lifanyike kwa utaratibu mzuri sababu bilioni moja kwa Wilaya moja ni fedha nyingi ndio maana nimesema itabidi zoezi baadaye likikubalika na Mheshimiwa Rais liwe ni jambo litakalofanyika awamu kwa awamu. Kwa hiyo, napenda nimthibitishie Mheshimiwa Simpasa pamoja na wananchi wa Mbozi kwamba litazingatiwa kikamilifu kabisa suala hili litakapokuwa limefikia wakati wake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Majimbo, kama nilivyosema nadhani na Waheshimiwa Wabunge wanajua kama si kwa sababu ya zoezi zito hili la Daftari la Kudumu, nina hakika kabisa baadhi ya Majimbo yangeweza kuzingatiwa kipindi hiki lakini maadamu zoezi hili limekamilika, naamini Ofisi ya Waziri Mkuu itakapokuwa imepata maombi haya kwa awamu inayokuja, nina hakika jambo hili litashughulikiwa ipasavyo.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwanza, kwa kuwa mimi binafsi nina hakika kwamba CCM itashinda na kuchukua madaraka ya Serikali, Waziri anaweza kututhibitishia rasmi lini utekelezaji wa kugawa Wilaya hizi utaanza?

Pili, kwa kuwa anafahamu kwamba Mkoa wa Rukwa sasa ni wa pili kwa ukubwa. Je, ugawaji wa Wilaya hizo kwa Mkoa wa Rukwa utazingatia Mkoa wote ili kutizama uwiano wa namna ya kupata Wilaya nyingi zaidi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kusema kwa uhakika ni lini jambo hili litatekelezwa ni vigumu kwa sababu mwenye mamlaka ya mwisho kabisa ya kuamua jambo hili ni Mheshimiwa Rais mwenyewe. Kwa hiyo, mimi nadhani kikubwa kwa upande wa ofisi yetu ni kwamba mradi kazi tumeikamilisha kwa maana ya uchambuzi jambo hili litawasilishwa kwa Mheshimiwa Rais yeye ataamua ni utaratibu upi aweze kuutumia. Kwa hiyo, nafikiri tufanye subira, nia ipo na wala hatukufanya uchambuzi wa Wilaya tu, tumejaribu kufanya hata uchambuzi wa Mikoa kwa lengo la kujaribu kufikia mahali ambapo tunaweza wote tukaona ina ahueni kiutawala.

Na. 12

**Mahitaji ya Umeme katika nchi za *SADC***

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA** aliuliza:-

Kwa kuwa, taarifa iliyotolewa kwa watendaji Wakuu wa *Southern African Power Pool* na kunukuliwa na gazeti la *Business Times* la tarehe 13/8/2004 linaonyesha kuwa mahitaji ya umeme katika nchi za *SADC* yataongezeka na itakapofika mwaka 2008 kutakuwa na upungufu wa umeme katika nchi hizo; na kwa kuwa, Mpango wa Taifa wa Umeme *(PSMP)* ulitegemea pia *Inter-connector* ya Zambia na Tanzania; na kwa kuwa, chanzo kikuu cha umeme wa Zambia ni umeme wa nguvu za maji kama ilivyo kwa nchi ya Tanzania:-

(a) Je, ni vizuri kuendelea na mpango huo wa kupata umeme wa Zambia, na kwamba, mpango huo hautatupotosha kwa siku zijazo?

(b) Je, isingekuwa vyema utekelezaji wa dhana ya *Inter-connector* ukasubiri kuanza au kuondolewa kwenye mipango yetu kwa sababu tutapoteza fedha nyingi katika kufanya maandalizi yake?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Daimon Mwaga, Mbunge wa Kibakwe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa katika nchi za *SADC* mahitaji ya umeme yataongezeka na kuzidi uwezo wa sasa wa kuzalisha umeme ifikapo mwaka 2008. Sambamba na kukua kwa matumizi, mipango kabambe ya kuongeza uzalishaji wa umeme inaandaliwa. Taasisi ya *SAPP* imeandaa miradi mipya ambayo itakuwa inazalisha umeme kwa kutumia vyanzo mbalimbali katika nchi wanachama yenye uwezo wa kuzalisha Megawati 8,544 zaidi ifikapo mwaka 2010. Ni vizuri nchi yetu iendelee na mipango ya kuunganisha gridi yetu na gridi ya Zambia ili kuongeza uwezekano *(accessibility)* wa kupata umeme wa gharama nafuu kutoka nchi wanachama wa *SAPP.* Aidha, mpango huu unatoa nafasi kwa Taifa letu ya kuendeleza vyanzo vyetu ikiwemo Mchuchuma ili kuweza kuuza ziada itakayokuwa inapatikana katika soko kubwa kuliko kutegemea soko la nchini tu.

(b) Mheshimiwa Spika, uunganishaji wa gridi za umeme katika nchi jirani na za kikanda ni hatua muhimu katika kujenga uchumi imara, unaotabirika na ambao hautegemei kudra za Mwenyezi Mungu katika kupatikana mvua za kutosha. Mradi wa *Inter-connector* kati yetu na Zambia, hatimaye Kenya, Uganda na nchi nyingine zinazoshiriki katika *SAPP* ni kiungo muhimu katika kuleta mapinduzi katika kuendesha uchumi wetu kwa misingi iliyo endelevu.

Hivyo, siyo vema kusitisha mpango huu, bali Serikali itaendelea kushirikiana na washirika wenzake pamoja na wadau muhimu katika kufanikisha hili.

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Spika, nina maswali madogo mawili.

(a) Kwa kuwa sasa hivi Tanzania haina mchango wowote katika hii *Inter-connector* kwa sababu haina umeme wa kutosha na uliopo ni wa bei kubwa. Je, kama Tanzania itakuwa katika huu mpango wa *Inter-connector* si itakuwa mpagazi wa umeme kutoka Zambia? Waziri anasema nini juu ya hili la upagazi?

(b) Kwa kuwa uchumi wa nchi za *SADC* unaongozwa na Afrika Kusini ambako 90% ya umeme wake ni wa mkaa wa mawe. Je, sisi Tanzania tunajifunza nini katika uzoefu wa Afrika ya Kusini? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, swali kuhusu umeme kutoka Zambia kuunganishwa na umeme wa Tanzania na hatimaye Kenya na nchi nyingine za jirani, ni jambo la msingi sana.

Mheshimiwa Spika, umeme ni bidhaa ambayo inauzwa na kununuliwa kama bidhaa nyingine yoyote ile.

**MBUNGE FULANI:** Alaaah.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Sisi tunazo rasilimali ambazo zinaweza kuzalisha umeme mwingi sana kuliko mahitaji yetu. Lakini sababu mojawapo iliyotufanya tusizalishe umeme huo au wawekezaji wasipatikane kuzalisha umeme huo ni kwamba hatuna soko la kutosha na hatuna njia za kuweza kuufikisha umeme huo katika masoko kule waliko.

Tukiunganishwa na Zambia na Kenya tutakuwa na njia hizo na umeme tunaweza kuuzalisha wa kwetu tukawauzia wenzetu *South Africa* ambao watapungukiwa na umeme ifikapo mwaka 2010 lakini Kenya kwa mfano sasa hivi wanangoja umeme hatuna *Inter-connector* tunajaribu kuunganisha Arusha na Nairobi ili umeme wetu ambao tutakuwa tunauzalisha kutoka kwenye gesi tuliyonayo ule wa ziada tuweze kuwauzia wenzetu wa Kenya. Ni biashara ambayo itatuletea fedha za kigeni na kutusaidia kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu hali ya umeme *South Africa* ni kweli lakini *South Africa* wanategemea sana makaa ya mawe na sisi tunaamini sisi tuna makaa ya kutosha ya kuzalisha umeme kule Mchuchuma lakini kama nilivyosema hakuna mwekezaji atakayekuja kuwekeza ikiwa hakuna soko ambalo ni la uhakika litakalonunua umeme huo.

Kwa hiyo, tumejifunza kutoka *South Africa* kwamba makaa ya mawe ni chanzo kizuri cha kuzalisha umeme na sasa hivi tuko katika hatua za kuzungumza na wawekezaji ili waweze kuendeleza na kuzalisha umeme pale Mchuchuma.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri tumeshaanza, umeme kidogo, umeme kidogo na kwa kuwa sisi watu wa Mtwara na Lindi tuna wasiwasi kwamba gesi yetu ya *Mnazibay* mtatafuta sababu ya kuipeleka Ubungo tena. Je, utatuhakikishia hapa Mheshimiwa Waziri gesi yetu ya *Mnazibay* umeme wake ni Mtwara na Lindi tu kama mlivyotuahidi, maana yake mmeshaanza hapa. *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia yeye na wananchi wa Mtwara na Lindi kwamba kwa kweli mpaka sasa hivi mradi wa kuzalisha umeme kutoka gesi ya *Mnazibay* unaendelea vizuri. Wameshafanya *test* za kwanza imeonekana ipo gesi ya kutosha kabisa lakini zuri zaidi ni kwamba wale wawekezaji wameshaanza kutoa tenda za kujenga gridi kutoka pale gesi ilipo ambapo umeme utazalishwa kwenda mpaka Masasi katika hatua ya kwanza. Kwa hiyo, Mheshimiwa Namkulala wewe na Mheshimiwa Watondoha na wananchi wa Mikoa

ya Kusini ninyi mlioko Bungeni naomba bajeti yangu mwaka huu 2005 muipitishe na wananchi watapata umeme wao kabla ya mwisho wa mwaka ujao. *(Kicheko)*

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa chanzo cha umeme Tanzania tunachotegemea ni maji na maji duniani na hata Tanzania yanapungua na kwa kuwa maji yanategemewa sana na kilimo kisichokuwa na mbadala. Je, mipango yetu Tanzania tunasemaje, tunaiangalia vipi hali hiyo ili tupate umeme wa uhakika na hasa umeme wa Mchuchuma? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli umeme wetu unatokana na maji kwa kiasi ambacho kilifikia 80% kwa miaka michache iliyopita lakini sasa utegemezi huo umepungua kwa sababu gesi yetu hasa ya songosongo imeanza kuingia kwenye gridi na sasa hivi inazalisha karibu *megawatt 185* na inaweza kufika 200 na bado tunaweka *generator* nyingine ili tuweze kutumia gesi hiyo kwa kiwango kikubwa zaidi kwa sababu gesi ipo, bomba lipo na inaweza kutumika kwa kazi hiyo.

Kwa hiyo, utegemezi wa maji unapungua lakini tukumbuke kwamba maji kwa kweli ndio chanzo rahisi kabisa kwa sababu maji ni ya Mungu yakipatikana pale yalipo yanaweza kuzalisha umeme kwa bei nafuu sana. Tunategemea gesi yetu kwanza kama ninavyosema wawekezaji wapo ambao tunajaribu kuwashawishi na kuzungumza nao waweze kuzalisha umeme kutokana na makaa ya mawe kule Mchuchuma vyanzo vingine ni kama jua, upepo kama kuna mwekezaji yeyote ambaye mnamfahamu nchi nyingine zinazalisha umeme mwingi sana kutokana na jua na upepo ninyi Waheshimiwa Wabunge kaleteni wabia kutoka India, Ulaya, tutawapa leseni mzalishe umeme wa aina hiyo na nchi yetu ipunguze utegemezi wa maji na mvua.

Na. 13

**Maombi ya Uchimbaji wa Madini**

**MHE. DR. LAWRENCE M. GAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa maombi ya wachimbaji wakubwa wa madini yanaingilia maombi ya wachimbaji wadogo wa madini kwa namna isiyoeleweka:-

(a) Je, ni lini Serikali itachukua hatua ya kufuta maombi ya wachimbaji wakubwa ili kutoa leseni za uchimbaji *(PMLS)* kwa wachimbaji wadogo wadogo wa Kitai Mkoko, Masuguru, Amani Makoro?

(b) Kwa nini Serikali hailitolei uamuzi shauri hilo ambalo limechukua muda mrefu sana?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Dr. Lawrence Gama, Mbunge wa Songea Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kuona matatizo kati ya wachimbaji wadogo na wakubwa wa maeneo ya Kitai, Mkoko, Masuguru na Amani Makoro Wilayani Mbinga niliagiza Kamati ya Ushauri ya Madini iende Mkoani Ruvuma kusikiliza pande zote zinazohusika katika malalamiko ya wachimbaji wadogo na baadaye inipatie mapendekezo.

Ikiwa Mkoani Ruvuma, mwezi Januari mwaka huu, Kamati ilikutana na Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Magereza wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya ya Mbinga, wachimbaji wadogo na Mkurugenzi wa kampuni yenye leseni kubwa ya kuchimba vito ya *World Gems Supplies Limited.* Kamati iliporudi Dar es Salaam ilikutana na kujadili yaliyojitokeza katika mahojiano na wadau Mkoani Ruvuma na kuliangalia suala hili kwa undani kwa kuzingatia Sheria ya Madini ya mwaka 1998 ili iweze kunishauri na kutoa uamuzi.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Madini ya mwaka 1997 na Sheria ya Madini ya mwaka 1998 zinawatambua watafutaji na wachimbaji wadogo na wakubwa wa madini, hivyo kufuatia ushauri wa Kamati, uamuzi sahihi utatolewa kwa kuzingatia sheria. Iwapo itabainika kuwa wenye leseni za utafutaji madini wameshindwa kuyafanyia kazi maeneo waliyopewa kama inavyotakiwa kisheria, Wizara yangu itawachukulia hatua wale watakaoshindwa kufuata masharti ikiwemo kuwafutia leseni na maeneo yatakayokuwa wazi yatatengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo wa madini.

**MHE. DR. LAWRENCE M. GAMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja tu la nyongeza.

Kwa kuwa suala hili limechukua muda mrefu kidogo. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kunithibitishia ni lini uamuzi wake utatolewa katika suala hili?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli suala hili limechukua muda mrefu kwa sababu ya unyeti wake, wachimbaji wakubwa, wachimbaji wadogo na sio mmoja tu ni wengi. Lakini nimhakikishie tu kwamba Kamati imesharudi na imeshatoa ushauri wake na nitatoa uamuzi kabla ya Bajeti yangu ya mwezi ujao.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, tatizo lililopo Songea kuhusu wachimbaji wadogo na wakubwa linafanana sana na tatizo lililopo Lwamgasa, Nyakagwe na Nyarugusu kwa manyanyaso wanayopata wachimbaji wadogo kwa sababu wachimbaji wakubwa wanachukua maeneo makubwa na wanayakalia wanasema wanafanya uchunguzi wanachukua muda mrefu sana na wanaporudisha wanayachukua hayo hayo. Je, Serikali ina utaratibu gani kuweza kuyachukua maeneo hayo ili wapewe wachimbaji wadogo ambao wanaweza kuendelea na kazi ya uchimbaji badala ya kuendelea kusubiri wakati wachimbaji wakubwa hawafanyi kazi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli utafutaji wa madini ukifanywa na wakubwa au wadogo unachukua muda mrefu na fedha nyingi sana, na ni kweli kwamba kuna wakubwa wengine ambao wakishapata leseni aidha kwa sababu hawajapata fedha mapema au ule utafutaji umechukua muda mrefu kwa sababu hawajayaona hayo madini basi inaonekana kama wamekalia maeneo kwa miaka mingi sana.

Mheshimiwa Spika, lakini sheria yetu inasema leseni ikitolewa baada ya miaka fulani kama hukufanya lolote pale tunafyeka lile eneo kwa nusu hata watafutaji wa mafuta na gesi ni hivyo hivyo ili usikalie eneo kubwa bila kuliendeleza ikipita miaka mingine tena ile nusu iliyobakia tunaipunguza kwa nusu tunawapa wengine. Sasa kama kuna wachimbaji wadogo wadogo ambao wako tayari wakati huo kutafuta madini pale, Serikali itawapa kipaumbele ili waweze kuyatafuta madini hayo na kujipatia riziki yao.

Na. 14

**Mauaji ya Waafrika**

**MHE. JOHN L. MWAKIPESILE** aliuliza:-

Kwa kuwa, karibu miaka mia mbili iliyopita Waafrika weusi walipata mateso makubwa kwa kushikwa bila ridhaa yao na kuuzwa kama bidhaa kwa wafanyabiashara wa Mataifa ya nje hususani Marekani na Uarabuni; na kwa kuwa hivi sasa hisia za uonevu huo wa Waarabu dhidi ya Waafrika weusi zimeanza kuibuka hasa nchini Sudan ambako Waafrika weusi wanauawa na maelfu ya wanamgambo wa Kiarabu wakisaidiwa na Serikali yao:-

(a) Je, ni kwa nini Umoja wa Afrika uko kimya juu ya mauaji ya Waafrika Jimboni Darfur, Sudan wakati umoja huo huo wakati ule ukiitwa *OAU* uliipinga vikali Serikali ya Makaburu wa Afrika Kusini juu ya udhalimu wake dhidi ya Waafrika weusi nchini humo?

(b) Je, ni kwa nini Serikali ya Tanzania iko kimya kinyume na kawaida yake juu ya mauaji hayo ya kikatili ambapo maelfu ya wanawake na watoto wameuawa baada ya kufanyiwa vitendo viovu?

(c) Baada ya biashara ya utumwa kupigwa marufuku miaka mia mbili iliyopita, Waafrika waliojikuta wako Amerika bado wapo huko mpaka leo. Je, Waafrika waliouzwa na kwenda Uarabuni waliishia wapi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali Na.14 la Mbunge wa Kyela, Mheshimiwa Mwakipesile, lenye sehemu a, b na c kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ningependa kuungana na Mheshimiwa Mwakipesile kwa kukiri kwamba biashara ya utumwa ilikuwa ovu iliyosababisha mateso makubwa siyo tu kwa watu wa Afrika bali pia kwa watu wa Mabara mengine.

Kwa msingi huo, wote walioshiriki kwenye biashara hiyo ikiwa ni pamoja na wanunuzi wa watumwa na mawakala wao ambao kwa upande wa Afrika miongoni mwao walikuwa watawala wa makabila mbalimbali, wanastahili kulaumiwa na hata kulaaniwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba biashara hiyo ilishapigwa marufuku duniani kote miaka 200 iliyopita, ni kweli kwamba kuna taarifa za biashara hiyo kuendelea kwa namna mbalimbali sehemu kadhaa duniani. Katika Bara la Afrika, kuna madai kuwepo biashara hiyo kichinichini katika nchi kadhaa za Afrika Magharibi na Mashariki mwa Afrika.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ushirikiano wa dunia kupitia mikataba mbalimbali ya Kimataifa dhidi ya biashara ya utumwa, kuna matumaini kwamba hatimaye biashara hii haramu itafutika kabisa duniani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, ninaomba sasa kujibu vipengele a, b na c vya swali la Mheshimiwa Mwakipesile, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Umoja wa Afrika umekuwa mstari wa mbele siyo tu kukemea na kulaani mauaji na mateso huko Darfur na Sudan kwa ujumla bali pia umekuwa mstari wa mbele kusaidia kutatua mgogoro wa Darfur tangu ulipoanza. Juhudi hizo ni pamoja na kushawishi pande zinazohusika na mgogoro huo kuzungumza na kutia saini mkataba wa kusitisha mapigano uliosaniwa tarehe 10 Aprili, 2004.

Mheshimiwa Spika, Umoja wa Afrika bado unaendeleza juhudi za kutatua mgogoro wa Darfur. Mwenyekitiwa Umoja huo ambaye hivi sasa ni Rais wa Nigeria, Mheshimiwa Olesegun Obasanjo, hivi sasa anaongoza vikao vya usuluhishi kati ya Serikali ya Sudan na makundi yanayozozana kwa nia ya kupata ufumbuzi wa kudumu.

Hivi karibuni Umoja wa Afrika umemteua mwanadiplomasia aliyebobea wa Tanzania, Mheshimiwa Dr. Salim Ahmed Salim, kusaidia juhudi za usuluhishi huko Darfur. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Umoja wa Afrika kwa kushirikiana na Jumuiya ya Kimataifa hasa Umoja wa Mataifa unaendelea na juhudi za kumaliza mgogoro wa Darfur ikiwa ni pamoja na kuwahudumia waathirika wa mgogoro huo.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali ya Tanzania haijawa kimya kuhusu mgogoro wa Darfur. Msimamo wetu wa kutopendezwa na kinachotokea Sudan tumeufikisha kwa viongozi wa Sudan na wao wanaufahamu na kutuelewa. Siku zote Tanzania imekuwa

ikishirikiana na Umoja wa Afrika pamoja na Umoja wa Mataifa na Taasisi zake mbalimbali katika kukemea na kulaani mauaji pamoja na kutafuta suluhisho la kudumu la mgogoro wa Darfur. Wakati huo huo, hata hivyo, Tanzania imekuwa ikishiriki vilivyo kutafuta suluhisho la amani huko Darfur.

(c) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba biashara ya utumwa imepigwa marufuku miaka mia mbili iliyopita na ni kweli kwamba vizazi vya watumwa waliouzwa Marekani bado vipo hasa huko huko Marekani. Hii inatokana na ukweli kwamba watumwa wengi waliotoka Afrika pamoja na wale waliotoka Afrika Mashariki waliishia Bara la Marekani. Hali kadhalika vizazi vya wale waliouzwa Uarabuni bado wako huko mpaka leo. *(Makofi)*

**MHE. JOHN L. MWAKIPESILE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Vile vile, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Ninalo swali moja.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje anao uzoefu mkubwa katika mambo na masuala ya nje na Ushirikiano wa Kimataifa na kama alivyosema yeye pale Chimwaga tarehe 4 mwezi uliopita, kwamba sasa anao uwezo mkubwa wa kutambua nchi inayotawaliwa vizuri na nchi inayotawaliwa vibaya:-

(i) Je, Waziri atakubaliana na mimi kwamba Sudan ni moja ya nchi katika Afrika ambayo inatawaliwa vibaya?

(ii) Kama anakubaliana na mimi katika swali la kwanza; Je, kwa nini Serikali ya Tanzania haijavunja uhusiano wa Kidiplomasia na Sudan, nchi ambayo inauwa wananchi wake kwa misingi ya udini, ukabila na rangi ambayo ni kinyume kabisa na itikadi na imani yetu katika Chama chetu cha CCM, ambacho Waziri Kikwete, baada ya miaka miwili kutoka sasa atakuwa ndiyo Mwenyekiti? (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Serikali ya Sudan imekuwa ikilaumiwa na baadhi ya Taasisi mbalimbali hasa Mashirika yasiyokuwa ya kiserikali kwamba suala hili la biashara ya utumwa linaendelea. Serikali ya Sudan imekuwa ikikanusha. Hali kadhalika katika mgogoro huu wa Darfur kumekuwa na matatizo ya watu kupigana wenyewe kwa wenyewe na kumekuwa na shutuma vile vile kwamba mapigano hayo ni ya kikabila au kidini.

Mimi mwenyewe nilipata nafasi ya kwenda Sudan na kuzungumza na Viongozi wa Sudan ikiwa ni pamoja na Viongozi kutoka sehemu ya Darfur na walisema kwamba sio kweli kama mapigano hayo ni ya kidini au kikabila hasa Darfur. Kwa sababu watu wa Darfur karibu asilimia 99 ni Waislamu na wote wanazungumza Kiarabu. Kwa hiyo, siyo kweli kwamba mauwaji au mapigano hayo ni ya kidini na weusi; Wasudan wengi karibu wote ni weusi.

**WABUNGE FULANI:** Hata Rais mwenyewe mweusi!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Sasa sidhani kwamba ni suala la rangi au suala la kikabila au dini, ingawa wapo watu ambao wanapiga kelele kwamba ugomvi huo upo katika misingi hiyo. Sasa kama ingelikuwa kweli mapigano hayo kwa kweli hasa ni ya kikabila yakimbali na kidini Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika ungerifanya uchunguzi wake na kutoa kauli kwamba hivyo ndivyo ilivyo. Kwamba Umoja wa Mataifa haukotoa taarifa yoyyote kwamba mapigano hayo ni ya aina hiyo, lakini ninakiri kwamba ni mapigano mabaya, maovu ambayo yanaangamiza watu sio rahisi kusema kwamba mapigano hayo ni ya kikabila.

Mheshimiwa Spika, kwa ajili hiyo nasema kwamba, mgogoro wa aina hiyo hautatanzuka kwa Tanzania kufunga uhusiano na kukata uhusiano na Sudan, bali ni ku-*engage* Sudan kupitia katika Taasisi za Kimataifa, kupitia katika *AU* na sisi wenyewe kukaa nao pembeni na kila inapopatikana nafasi kusihi tatizo hilo litanzuliwe hara iwezekanavyo.

**SPIKA:** Sijui kama Mheshimiwa Waziri mwenyewe una majibu ya nyongeza.

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naomba niulize swali moja tu dogo la nyongeza. Kwa kuwa katika majibu yake, Mheshimiwa Naibu Waziri amekubali kwamba hawa watu walionunua wenzao katika Afrika Mashariki ni Waarabu na historia inatauonyesha hata majina ya hawa watu na ukifika Zanzibar unaona hata masoko yaliyotumiwa na hao Waarabu. Sisi kwa historia tunawajua hawa wanunuzi walitoka wapi, wakina Tip Tipu hawa. Sasa si halali kwa Serikali yetu kudai fidia kwa sababu walitunyang'anya nguvu kazi na kudumaza maendeleo ya nchi yetu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, utakumbuka kwamba mwaka 2001 kulifanyika Mkutano Mkubwa wa Kimataifa kule Durban ambao ulizungumzia masuala ya ubaguzi wa rangi, masuala ya ubaguzi wa kijinsia pamoja na matatizo yote yanayofungamana na ubaguzi ikiwa ni pamoja na utumwa. Katika miito mbalimbali iliyotolewa na maazimio baadaye kupitishwa ni kwamba nchi zilizoathirika zilitaka mambo kama mawili makuu.

(i) Kwamba nchi zilizokuwa zimehusika na biashara ya utumwa zikiri kwanza kwamba tendo lile lilikuwa ni ovu ni baya na halina buni kulaaniwa.

(ii) Mataifa ya Afrika hasa yalitaka palipwe fidia, yalipwe na aina zozote zile za kufutafuta machozi. Nchi nyingi ambazo zimekuwa zikishutumiwa kuhusika na biashara hii zilikuwa na hoja kwamba wakati zinakubali kukiri ya kwanza ya kulaani na kwamba tatizo hili lilikuwa ni ovu, zilikuwa na mashaka kuhusu vipi ingeweza kutekeleza suala la ilipaji fidia. Kwa sababu unaweka thamani vipi unakadiriaje, yote hayo yalikuwa ni matatizo makubwa.

Kwa hivyo hatimaye ikakubalika katika maazimio yale kwamba nchi hizo pamoja na nyingne zifanye mambo kadhaa, miongoni mwake ni kusaidia masuala ya maendeleo kwa kasi kubwa zaidi, kusaidia ujenzi wa miundo mbinu, kusaidia kufuta madeni, kusaidia kufungua masoko yao kwa bidhaa za nchi zinazoendelea na mambo mengine ikiwa ni pamoja na suala la Utawala Bora, kusaidia kuimarisha haki za binadamu na mambo ya elimu, mambo ya afya na kadharika.

Kwa hivyo hatimaye ilikubalika kwamba mambo hayo yatekelezwe kwa aina hiyo, badala ya kwenda kulipa fidia, kwa sababu haijulikani fidia hiyo angelipwa nani hasa mtu binafsi au ina thamani gani na itolewe vipi.

Na. 15

**Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza:-

Kwa kuwa yapo mambo kadhaa yaliyokubaliwa na viongozi wa juu wa Nchi Wanachama wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki yatekelezwe ili kuongeza ufanisi na baadhi ya mambo hayo ni pamoja na uteuzi wa Mawaziri na Manaibu Mawaziri wake kutoka katika Nchi Wanachama wa Jumuiya hiyo, na kuboresha Makao Makuu ya Jumuiya hiyo yaliyoko huko Arusha; na kwa kuwa, Kenya ndiyo nchi pekee iliyokwishateua Mawaziri na Manaibu Waziri wake:-

(a) Je, ni sababu gani zinazoifanya Tanzania isiwe na Waziri katika Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki hadi sasa ikizingatiwa kuwa uteuzi wake hauambatani na uchaguzi wake kama Mbunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(b) Kwa kuwa, Makao Makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yapo Arusha na upo mpango wa kuendeleza Makao hayo unaohitaji ongezeko la Ardhi; Je, Tanzania imewahi kuombwa ardhi kwa ajili ya mpango huo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mntangi, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Tanzania kama zilivyo nchi za Kenye na Uganda zinaye Waziri katika Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Waziri huyo ni yule mwenye dhamana ya kuratibu shughuli za Jumuiya katika Serikali. Kwa sasa Waziri huyo ni Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa

Kimataifa, kwa upande wa Tanzania. Uganda inawakilishwa na Waziri wa Mambo ya Nje na Kenya inawakilishwa na Waziri wa Ushirikiano wa Kanda. Jumuiya ya Afrika Mashariki na utaratibu huo hivi sasa utabadilika kufuatia uamuzi wa tarehe 30 Mei, 2005 wa Wakuu wa Nchi wanachama wa Jumuiya kuwa kila nchi iteue Waziri ambaye atashughulikia masuala ya Jumuiya peke yake.

(b) Mheshimiwa Spika, mwanzoni mwa mwaka huu 2005, Jumuiya ya Afrika Mashariki, imeshawasilisha maombi ya kupatiwa eneo kubwa la kujenga Makao Makuu ya Shirikisho la Afrika Mashariki. Katika mwaka 1996, iliyokuwa Tume ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki iliomba eneo kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu yake. Serikali ya Tanzania ilishatoa eneo la ekari 11 ambazo hivi sasa zitatumika kujenga Makao Makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kuhusu maombi ya eneo la kujenga Makao Makuu ya Serikali ya Shirikisho, Serikali ya Tanzania imeshakubali kimsingi na kwa sasa maeneo mawili yameshatambuliwa na mazungumzo yanaendelea kati ya Serikali na Sekretarieti ya Jumuiya kuhusu eneo muafaka. Mara maafikiano yatakapofikiwa Serikali ya Tanzania itatoa eneo hilo kwa matumizi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**MHE. HERBERT MNTANGI:** Mheshimiwa Spika nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, hata hivyo nina maswali madogo mawili ya nyongeza:-

(a) Kwa kuwa upo utaratibu wa *Fast Track* unaoelekeza utekelezaji na uboreshaji wa uwendelezaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Je, ni lini sasa kwa ratiba ya *Fast Track* uteuzi wa Mawaziri hawa wa Shirikisho la Jumuiya ya Afrika Mashariki utafanyika?

(b) Kwa kuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki sasa inaelekea katika kafunguwa mipaka na hivyo kuruhusu wafanyakazi pamoja na wafanyabiashara kupita katika nchi kwa uhuru na kwa kuwa hatua hiyo itakuwa inahusu utumiaji wa ardhi, ardhi ambayo ni mali ya wananchi, wanavijiji wetu. Je, Serikali inautaratibu gani sasa wa kutoa elimu kwa wanavijiji hao ili waweze kujua faida na hasara ya kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, katika azimio la pamoja lililotolewa na viongozi tarehe 30 mwezi uliopita hawakuweka tarehe maalumu ya lini Mawaziri hao wateuliwe. Walichofanya katika suala hili kubwa ni mambo mawili. Moja ni kuagiza Baraza la Mawaziri liweke taratibu mbalimbali za kutafuta mawazo na maoni ni vipi suala la kuharakisha kupatikana shirikisho lingeweza kupata mawazo mbalimbali na baadaye katika miezi kumi na mbili ifuatayo waweze kutoa maoni yao kwa viongozi.

Sasa ni matumaini yangu kwamba, katika utaratibu huo wa kupanga vipi suala zima hili lingeweza kupata maoni na mawazo, Mawaziri wataweza kukaa kitako na kuangalia kutazama jinsi gani na utaratibu gani ufanyike katika kupatikana Mawaziri.

Mkataba wa kuanzishwa Jumuiya ya Afrika Mashariki kipengele cha 13, kinazungumzia kwamba kutakuwepo Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki na kutakuwepo Mawaziri watatu, mmoja kutoka katika kila nchi mwanachama ambao watakuwa na jukumu la Ushirikiano wa kanda, imeishia hapo na kwamba Baraza hili la Mawaziri litaweza kujumuisha Mawaziri wengine wowote wale ambao kila nchi husika itaamini kwamba angefaa kuwemo katika Baraza hilo kwa mujibu wa Sekta yake.

Lakini haizungumzii Waziri huyu wa sasa ambaye amependekezwa na ameagizwa na viongozi kwamba awepo Waziri atakaye shughurikia masuala ya Jumiya tu.

Sasa natumai kwamba katika muda utakaofuata huu, Mawaziri kwa kupitia *levels* mbalimbali za ushauri wanaoupata kutoka kwa Makatibu Wakuu na kadharika, hayo ni miongoni mwa masuala ambayo yatabidi kuzungumzwa kwa kina kutafuta njia gani Waziri aweze kupatikana akishapatikana je, hata Wanasheria wanaweza ikabidi na wao watoe ushauri wao kama pengine patahitajika kuwepo Katiba ya Jumuiya Afrika ya Mashariki ifanyiwe mabadiliko.

Haya yote ni masuala yanayohitaji muda, ninachoweza kusema kwamba itafanywa haraka iwezekanavyo lakini lazima kupitia njia mbalimbali ili kuepuka migongano au kuwepuka mambo ambayo yanaweza yakatokea baadae, badala ya kusaidia kuharakisha na Waziri huyu akaweza kufanya kazi yake itakiwavyo na ipasavyo asije akawa tatizo katika utekelezaji wake.

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona...

**SPIKA:** Samahani Mheshimiwa Marmo, tafadhali, Mheshimiwa Waziri ambaye Uwaziri wake unakwisha tarehe 30 Oktoba, 2005 ana majibu ya nyongeza. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa maelezo ya ziada kama ifuatavyo:-

Kwanza, hili la Mawaziri, uteuzi unategemea uamuzi wa Marais maana wamekwisha kubaliana wenyewe wateue Mawaziri, watakavyoamua itakuwa hiyo ni uamuzi wa Marais wa Nchi zetu tatu.

Hili la ardhi ambalo Mheshimiwa Mbunge amelielezea, ni moja ya jambo ambalo katika mazungumzo yale ya *Fast Track,* upande wa Tanzania tulilizungumzia sana kwamba ni eneo *of concern.* Na mtakaposoma ile Ripoti na ndiyo maelewano yaliyotokea ni kwamba suala la ardhi halitafanywa kuwa ni ardhi ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Ardhi itabakia kwamba ni ardhi ya nchi Wanachama na nchi wanachama ndizo zitakuwa na mamlaka ya kuamua nani atahamia na nani atakaa wapi na nani hatahamia. Kwa hiyo, hili tusiwa wasiwasi nalo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na hasa majibu ya Mheshimiwa Waziri, nataka kuuliza swali la nyongeza linalosema kwamba; kwa vile mchakato wa Shirikisho letu hatimaye utahitaji Mji mzuri, Mji wa kisasa kabisa na kwa vile sasa Mji huu tulionao ni duni kwa kila hali: Je, Serikali haioni kwamba pamoja na kwamba ardhi itakuwa ya Tanzania, wakati umefika sasa wa kuunda chombo kama *CDA* ya Dodoma itakayosimamia uendelezaji wa Mji huu ili ukidhi mahitaji ya nchi za Afrika Mashariki na wananchi wake?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, tumepokea ujumbe huo, utazingatiwa na Wizara inayohusika.

Na. 16

***Surcharge* kwa waliofilisi *SACCOS-VUNJO***

**MHE. MAJOR. JESSE J. MAKUNDI:** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilipojibu swali Na. 29 katika Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge hapo tarehe 13 Aprili, 2005 ililiambia Bunge kuwa waliofilisi Vyama vya Ushirika, Akiba na Mikopo *(SACCOS)* vya Mamba, Mwika Kaskazini na Mashariki, Ngakoma, Marangu Mashariki na Magharibi na Legho- Mulo katika Jimbo la Vunjo, watapelekewa *Surcharge* kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2003 na kanuni zake za mwaka 2004:-

(a) Je, ni tarehe ipi mwezi na mwaka, gani watapelekewa *Surcharge* watuhumiwa hao kwa Sheria hiyo mpya ya mwaka 2003.

(b) Je, ni nani hao kwa majina na kutoa kwenye *SACCOS* ipi waliopelekewa *Surcharge* na ni hatua gani zaidi zilifuata kwa watuhumiwa hao ili waathirika waweze kurudishiwa fedha zao walizokuwa wameweka kwenye benki hizo.

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Meja Jesse Makundi, Mbunge wa Vunjo, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa nilipokuwa najibu swali lake Na. 29 katika Mkutano wa Bunge wa Kumi na Tisa nilieleza kusudio la Serikali la kuwapelekea *Surcharge* watuhumiwa wote waliohusika na ubadhirifu wa

fedha za Vyama vya Akiba na Mikopo alivyovitaja ili watuhumiwa hao watakiwe kufidia ubadhirifu wa fedha walioufanya katika vyama hivyo.

Kufuatia ahadi hiyo na kwa kuzingatia Sheria ya Vyama vya Ushirika ya 2003, Serikali ilianza kutekeleza azma yake hiyo kuanzia tarehe 20/5/2005 kwa kuwapelekea *Surcharge* watuhumiwa wafuatao kutoka Chama cha Akiba na Mikopo cha *Mwika North-East SACCOS.* Nawataja:-

1. Bwana Geoffrey Shao;
2. Bwana Ufurosia Makundi *;(Kicheko)*
3. Bwana Estomih Kimaro;
4. Bwana Geoffrey Msella;
5. Bwana Stanford J. Ngowi;
6. Bwana Kundasa Lyimo;
7. Bwana Julita L. Maanga;
8. Bwana Kauweli S. Samu;
9. Bwana Anael Mtei;
10. Bwana Elisaria Thomas Shao;
11. Bwana Jonathan Machange;
12. Bwana Stephano O. Shao; na
13. Bwana Azaria E. Massaule.

Kuhusu watuhumiwa wa *Ngakoma SACCOS,* Mrajisi bado anawasiliana na wanachama wa chama hicho kabla ya kutekeleza kusudio hilo kwa vile wanachama hao wa *Ngakoma SACCOS* walikuwa wameunda tume ya kuchunguza mwenendo wa chama chao. Baada ya taarifa ya Tume hiyo ya wanachama Mrajisi atatoa maelekezo ya kushughulikia tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Vyama vya Akiba na Mikopo vya *Mamba and Marangu-West* suala lao linashughulikiwa na Kitengo cha Upelelezi wa Makosa ya Jinai wa Mkoa wa Kilimanjaro; wakati Vyama vya *Marangu-East SACCOS* na *Legho-Mullo SACCOS* taarifa za ukaguzi hazikubainisha ubadhihirifu wowote katika vyama hivyo.

**MHE. MAJOR. JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kutoa majibu ambayo kwa kiasi fulani yanaridhisha. Lakini kwa kuwa kwa miaka yote mitano na sasa ndiyo mwisho wake na Waziri anaondoka madarakani. Je, yuko tayari kuwaachia kazi hiyo Wataalam, wakiwepo Mrajisi Mkuu, Katibu Mkuu wa Wizara ili aharakishe kuwakamata hawa wezi na hatimaye fedha ziweze kurudi na wale ambao walidhulumiwa waweze kupata haki zao?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba tunamaliza kipindi chetu cha uongozi hapa, lakini Serikali ipo, inaendelea kuwepo wakati wote. Kwa hiyo, hata haya niliyoyaeleza hapa, nataka kusema tuwaachie wataalam, Serikali imekuwa ikielekeza shughuli hizi zinafanywa kikamilifu na kwa vile

Serikali itaendelea kuwepo, hizi shughuli zote ambazo zimeishaanza kutekelezwa zitaendelea kushughulikiwa na kama nilivyokwisha kusema kwamba hawa wengine tayari wameishafikishwa kwenye vyombo vya Sheria kwa hiyo hatua za Kisheria zimeanza kushughulikiwa.

**SPIKA:** Ni vizuri tukajua Waheshimiwa Wabunge kwamba pamoja na kwamba Bunge litavunjwa mapema, lakini kwa mujibu wa Katiba yetu, Mawaziri wataendelea kuwa Mawaziri mpaka hapo Rais mpya atakapoapishwa. Kwa hiyo, bado wako madarakani, isipokuwa mmoja Yeye ataishia Tarehe 30 Oktoba, 2005. *(Kicheko)*

Na. 17

**Soko la Matunda**

**MHE. LYDIA T. BOMA** aliuliza:-

Kwa kuwa wakulima wanajitahidi sana kuzalisha mazao mbalimbali ya biashara na chakula yakiwemo matunda, lakini bahati mbaya hayana ubora wa kupata soko la nje:-

(a) Je, tatizo la ukosefu wa ubora wa mazao kuuzwa nje na kuhimili soko hilo linatatuliwaje na Serikali?

(b) Kwa kuwa Mkoa wa Mtwara unalima matunda mbalimbali kama vile maembe, machungwa, mananasi, mabibo na kadhalika. Je, Serikali itawapatia soko la ndani na nje kwa mazao hayo?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lydia Boma, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Katika jitihada za kutatua tatizo la ubora wa mazao yetu na kuweza kuhimili ushindani wa soko la nje, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, na Wadau wengine inawasaidia wakulima na wafanyabiashara waweze kuzalisha mazao yenye ubora unaostahili kwa kufanya mambo yafuatayo:-

Kwanza, Kutoa elimu kwa wakulima na wafanya biashara juu ya kuzalisha na kuuza mazao yenye ubora unaokubalika katika masoko ya ndani na nje ambapo mwaka 2004 Wizara yangu iliendesha warsha ya Kitaifa ya kukuza matumizi ya Soko la ndani na nje na mbinu za kuingia katika masoko hayo zilibainishwa. Aidha Wizara yangu imeendesha warsha mjini Mwanza na Zanzibar na zingine zinaandaliwa katika Kanda nyingine za kuelimisha wakulima na wafanyabiashara jinsi ya kuongeza mauzo ya bidhaa za Tanzania katika nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Pili, Kuhimiza Taasisi za Utafiti wa mazao ya kilimo kuendeleza na kusambaza mbegu na miche bora ya mazao yanayotakiwa kwa ajili ya masoko ya nje na ndani.

Tatu, Kuhamasisha kwa njia ya semina za mafunzo zinazoendeshwa na Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Masoko pamoja na Maonyesho ya Nane Nane, maonyesho ya kila mwaka ya siku ya Ushirika Kitaifa na mafunzo yatolewayo na Shirika la Viwanda Vidogo Vidogo *(SIDO).*

Nne, Kuwawezesha wazalishaji, wasindikaji na wafanyabiashara kushiriki katika maonyesho ya Kimataifa ili kujifunza mbinu za kuwezesha kupenya au kupanua masoko ya mazao yao katika masoko ya ndani na nje. Kwa mfano, mwaka 2004 Serikali iliwawezesha wazalishaji na wafanyabiashara wa mazao ya chakula kushiriki katika maonyesho ya mazao ya vyakula mjini Moscow kule Urusi.

Tano, Kuimarisha Miundombinu ya masoko ikiwa ni pamoja na ujenzi wa masoko ya kisasa kama vile Masoko ya Nyandira, Kinole na Tuwa Mkoani Morogoro, Kibaigwa Mkoani Dodoma na Tengeru Mkoani Arusha.

Aidha chini ya mradi wa kuendeleza Miundo mbinu ya Masoko maandalizi ya ujenzi wa masoko mengine 20 yanafanyika.

Sita, Kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara, imeanzisha mfuko ujulikanao kama *National Entrepreneurship Development Fund* na mwingine wa *Small and Medium Enterprise Credit Guarantee Fund* yenye lengo la kutoa dhama ya mikopo na kuendeleza ujasiriamali kwa Wafanyabiashara wadogo wadogo.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inasaidia wakulima wa matunda wa Mtwara na maeneo mengine nchini katika upatikanaji wa masoko ya ndani na nje kwa mazao yao kwa kuweka mazingira mazuri ya kibiashara yanayotoa nafasi kwa wazalishaji wa mazao hayo kuuza ndani na nje ya nchi. Baadhi ya mambo yanayotekelezwa na Serikali ni haya yafuatayo:-

La kwanza Kuimarisha vyama vya Ushirika na vikundi vya wazalishaji wadogo na wa kati katika masuala ya mitaji na elimu ya ujasiriamali na stadi za biashara kwa lengo la kuviongezea uwezo wa kuuza mazao yao wakulima katika masoko mbali mbali ikiwa ni pamoja na masoko maalum kama vile mahoteli na *Super Markets.*

Pili, kutoa elimu kwa Umma kwa kutumia njia mbalimbali nilizoeleza katika sehemu (a) ya suala hili.

Tatu, kuhamasisha wawekezaji ili wajenge viwanda vya kusindika matunda kama ilivyofanyika katika mikoa ya Morogoro, Arusha na Dar es Salaam. Na mwisho, kuhamasisha uwekezaji kwenye mashamba makubwa ya matunda kama vile mananasi, machungwa na maembe kwa lengo la kuwezesha wazalishaji wadogo wadogo kuingia katika kilimo cha mkataba kama njia ya uhakika ya kuzalisha mazao yenye ubora unao kidhi mahitaji ya soko.

**MHE: LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Spika ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri nina maswali madogo mawali ya nyongeza.

(i) Je, kwa nini Serikali mpaka sasa inaridhika uingizaji wa matunda kutoka nchi za nje na kusababisha matunda ya Tanzania kutokuwa na soko la ndani?

(ii) Kwa kuwa matunda ninayozungumza hasa ni ya wanawake wa Mkoa wa Mtwara wamekuwa wakulima na nina hakika kweli hawana soko. Je, Serikali ni lini sasa itawaletea kiwanda kikubwa cha kutengeza *Juice* kuliko sasa hivi tunatumia *Juice* ya kutoka nchi za nje?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, nadhani hata katika suala lenyewe alivyolielekeza mwazo pale ilikuwa ni kwamba mazao yetu hayana ubora unao stahili, na kutokuwa na ubora unao stahili ndiyo maana baadhi ya bidhaa kama hiyo ya matunda bado yanatoka nje kwa sababu yanakidhi ubora wa walaji hapa nchini. Lakini nikaeleza kwamba ili kuweza kukabiliana na hali hiyo ndiyo njia hizi mbalimbali nilizozieleza za kuweza kuyaboresha mazao yetu ili yaweze yakanunuliwa na wanunuzi hapa nchini na hatima yake hilo suala la kuagiza sasa mazao kutoka nje yatakwisha kwa sababu mazao yetu yatakuwa bora zaidi.

Mheshimiwa Spika. Lakini la pili la kusema kwamba Serikali itapeleka lini kiwanda, nilisema hapa kwamba Serikali imeandaa mazingira ya kuwezesha shughuli hizo zifanyike. Kwa hiyo Serikali haipeleki kiwanda, isipokuwa inaandaa mazingira ambayo yanawezesha wawekezaji pamoja na wafanyabiashara mbalimbali ambao wanaweza wakakidhi matarajio ya kuweza kuanzisha viwanda ili kuweza kukamilisha azma hii ambayo Mheshimiwa Mbunge ameiulizia.

Na. 18

**Sera ya Maendeleo ya Watu Wenye Ulemavu**

**MHE. MARGARETH AGNESS MKANGA** aliuliza: Kwa kuwa Sera ya maendeleo ya Watu wenye Ulemavu ilikuwa tayari tangu mwaka 2004:-

Je, ni lini Serikali italeta Mswada Bungeni ili kuwezesha utekelezaji wa yale yaliyo ndani ya Sera hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (k.n.y.WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO)** alijibu:

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margareth Agness Mkanga, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba Mwezi Machi, 2004 Serikali ilipitisha Sera ya maendeleo ya huduma kwa watu Wenye Ulemavu ambayo inalenga katika kujenga mazingira muafaka

kwa Watu wenye Ulemavu kujiletea maendeleo na kutumia rasilimali zilizopo kuboresha huduma kwao.

Utekelezaji wa Sera hii kwa hivi sasa hauhitaji kuandaliwa Muswada wowote na badala yake Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wote inakamilisha mkakati wa utekelezaji.

Pamoja na hali hii, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kutokana na umuhimu wake yapo masuala mbali mbali yaliyoingizwa katika utekelezaji wa Serikali hata kabla ya kukamilisha kwa mikakati hiyo.

Masuala hayo ni pamoja na marekebisho ya Sheria ya ajira na matunzo (Na. 1 na 3) za mwaka 1982 na kuridhia Kanuni za Umoja wa Mataifa kuhusu haki na usawa wa Fursa kwa Watu wenye Ulemavu.

Serikali pia inaendelea na jitihada za kuelimisha wananchi kuhusu nafasi ya Watu wenye Ulemavu katika jamii. Inatoa huduma za kinga dhidi ya magonjwa yanayoleta ulemavu kwa watoto walio chini ya miaka 5 na inaelimisha jamii na hasa akina mama wazazi kuhusu unyonyeshaji na lishe bora kwa lengo la kumkinga mtoto dhidi ya visababishi vya ulemavu.

Na. 19

**Mfuko wa *NSSF***

**MHE. KHAMIS AWESU ABOUD** aliuliza:-

Wafanyakazi wengi huwa wanakatwa fedha za *NSSF* kwa ajili ya mafao yakiwa ni malimbikizo ya makato hayo. Lengo kuu la makato hayo ni kuwa fedha hizo ziwasaidie wenyewe baada ya kustaafu kazi.

(a) Je, ni wafanyakazi wangapi wamejiunga na mpango huo?

(b) Je, ni wafanyakazi wangapi waliostaafu na kulipwa fedha zao?

(c) Kwa kuwa fedha hizo zinakusanywa na kuwekwa Benki na kwa kuwa Benki ina utaratibu wa kutoa riba kwa fedha zilizowekwa Benki, Je, fedha hizo watalipwa lini?

(d)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI) (k.n.y. WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO)** alijibu:

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud, Mbunge wa Mkanyageni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa mujibu wa Takwimu za Shirika la *NSSF,* hadi mwezi Machi, 2005, Mfuko una wanachama 346,142 ambao wamesambaa nchi nzima.

(b) Jumla ya shilingi Milioni 46.2 zinalipwa kama Pensheni kila Mwezi kwa wastaafu 994 waliokoma kufanya kazi kwa ajili ya umri wa kisheria.

Zaidi ya malipo hayo, mfuko umekuwa ukilipa wanachama wake wanaolazimika kuacha kazi kabla ya muda wa kustaafu kazi kwa sababu mbali mbali.

Kwa mwaka 2004/2005 hadi Aprili, 2005 jumla ya shilingi Bilioni 16.4 zimelipwa kwa wanachama 27,530 waliojitoa kabla ya umri wa kustaafu kisheria.

Pamoja na Pensheni ya kustaafu kwa umri, Mfuko pia hutoa mafao yafuatayo mwanachama anapokuwa kazini:-

- Mafao ya Uzazi;
- Mafao ya Kuumia kazini;
- Mafao ya Matibabu ambayo yataanza hivi karibuni.

(c) Riba inayopatikana katika fedha zilizowekwa katika Mabenki na Vitega Uchumi Vingine hugawanywa katika Akaunti za Wanachama wa Mfuko huo na pia fedha hizo hugharimia mafao yaliyotajwa hapo awali ambayo analipwa mwanachama yungali akiwa kazini na hayapunguzi mafao yake ya Pensheni za Ulemavu, Urithi au Kustaafu kazi.

**MHE. KHAMIS AWESU ABOUD:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa wapo wafanyakazi wa Zanzibar, wanaofanya kazi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa kuwa hawana Ofisi ya *NSSF* pale Zanzibar jambo ambalo linawafanya kuacha kazi au kufuatilia mfuko wao, kufuatilia mfuko Dar es salaam. Je, kwa nini Serikali haijengi Ofisi hapa Zanzibar ili kuwapunguzia matatizo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI) (k.n.y. WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO):** Mheshimiwa Spika, ni kweli wako wafanyakazi wachache wanaofanya kwenye Taasisi za Muungano ambazo ziko Zanzibar, na ni kweli kwamba hakuna Ofisi. Lakini jambo hili lilifanywa kwa makusudi kwasababu hata wao wenyewe ajira zao zinasimamiwa na Ofisi zilizoko Tanzania Bara. Hawa ni Watumishi, ingawa wanatoka Zanzibar lakini wanaweza kupangwa na kufanya kazi mahali popote katika Jamhuri ya Muungano. Kwa hiyo, kwa kweli kwa sasa Shirika halina mpango wa kujenga ofisi kwa sababu wale wafanyakazi wanahudumiwa na Kanda ya Pwani na Makao Makuu ya *NSSF* na hawajawahi kuwa na matatizo yoyote.

Na. 20

**Maiti zinazotelekezwa baada ya kufanyiwa Uchunguzi**

**MHE. MARIAM S. MFAKI** aliuliza:-

Kwa kuwa mara nyingi kumekuwa na vifo vinavyotokana na kuuawa, kujinyonga, kula sumu na kadhalika. Na kwa kuwa Polisi ndiyo wanahusika na uchunguzi wa matukio ya aina hiyo na baada ya hapo huchukua mwili wa Marehemu kwa Daktari kwa uchunguzi zaidi na baada ya uchunguzi huo wa Daktari Polisi mara nyingine huwa huzitelekeza maiti hizo ambao unakuwa mzigo wa familia husika na matokeo yake husababisha maiti kuzikwa katika maeneo ambayo hayakupendelewa na ndugu wa Marehemu kwa kushindwa kulipia gharama za usafirishaji:-

(a) Je, ni nani anahusika hapa katika kusafirisha maiti hao kupeleka kwao baada ya Polisi na Daktari kumaliza uchunguzi wao?

(b) Je, Serikali inasaidia vipi tatizo hilo kwa kuiwezesha familia husika kupata usafiri wa kusafirisha maiti wao kwao kwa mazishi baada ya uchunguzi kukamilika?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Mfaki, swali lake lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria za Jeshi la Polisi *(PGO)* Na. 224(5) inaelekeza kwamba inapotokea kuwa mtu kauwawa au kajinyonga au kunywa sumu na taarifa hiyo ikapelekwa katika kituo cha Polisi, Afisa wa Polisi humuarifu Daktari na wote kwa pamoja hufuatana kwenda kwenye eneo la tukio na kuchunguza maiti kwa madhumuni ya kubaini chanzo cha kifo hicho, na baada ya uchunguzi kukamilika maiti hukabidhiwa kwa ndugu wa Marehemu kwa ajili ya mazishi.

Inapotokea Daktari hakupatikana, Afisa wa Polisi huenda kwenye kituo peke yake na baada ya kumaliza uchunguzi huichukua maiti hiyo huipeleka Hospitalini kwa ajili ya uchunguzi wa Daktari. Baada ya Daktari kukamilisha uchunguzi wake, ni jukumu la Jeshi la Polisi kusafirisha maiti kutoka Hospitalini na kuirudisha kwa Ndugu wa Marehemu na kuwakabidhi kwa ajili ya mazishi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na wajibu huo wa Jeshi la Polisi wa kusafirisha maiti, wakati mwingine Jeshi la Polisi hushindwa kutimiza wajibu huo kutokana na kukosa usafiri, na katika mazingira hayo ndipo Idara zingine za Serikali au Ndugu wa Marehemu huombwa msaada wa kusafirisha maiti ili mwili wa Marehemu usiendelee kuharibika hospitalini. *(Makofi)*

Msaada huu unapoombwa isichukuliwe kuwa kero bali ni katika kudumisha Mila na Utamaduni wetu wa kushirikiana na kusaidiana nyakati za misiba.

Hata hivyo, kwa kadri Serikali inavyoliwezesha Jeshi la Polisi kuwa na vitendea kazi vya kutosha hasa magari, ndivyo litakavyo kuwa na uwezo zaidi wa kutoa huduma ya usafiri kwa Askari na raia wenye matatizo kama hili la kusafirisha maiti.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Mfaki, itabidi usamehe swali la nyongeza kwa sababu muda wa maswali umekwisha.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na *Order Paper,* labda niseme tu kwamba tumeshaanza kupokea karatasi za maombi ya kuchangia bajeti ingawa kwa mujibu wa ratiba yetu majadiliano ya bajeti yataanza keshokutwa tarehe 10, lakini maombi yanapokelewa tu yataorodheshwa na Makatibu Mezani. Tunaendelea na *Order Paper.*

## HOJA ZA SERIKALI

### Hoja ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2004 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2005/2006.

**SPIKA:** Sasa tunamwita Mtoa hoja ,Waziri mwenye dhamana ya Mipango na Ubinafsishaji ili awasilishe Hali ya Uchumi kwa mwaka wa fedha ujao. Namwita Mheshimiwa Waziri Mtoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likae kama Kamati ili liweze kupokea na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2004 na Mapendekezo ya Mpango wa Muda wa Kati na Mfumo wa Matumizi ya Serikali kwa kipindi cha mwaka 2005/06 - 2007/08. Pamoja na hotuba hii, nawasilisha Kitabu cha Hali ya Uchumi katika mwaka 2004 na kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha salama katika kipindi kingine cha kutoa taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa inayotokana na utekelezaji wa Serikali ya Awamu ya Tatu inayoongozwa kwa hekima na busara za Rais wetu Mpendwa Mheshimiwa Benjamin William Mkapa. Wengi wetu tumejifunza mengi chini ya uongozi huu wa Serikali ya Awamu ya Tatu. Hatuna shaka kuwa mafanikio yaliyopatikana yataendelea kukipatia Chama Cha Mapinduzi ushindi wa kishindo ili kiendeleze mazuri yote yaliyoanzishwa kwa lengo la kukuza uchumi na kuondoa umaskini nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Uchumi na Fedha ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mhe. Njelu Kasaka Mbunge wa Lupa kwa kujadili na kutupa ushauri pamoja na changamoto zilizochangia katika kuboresha na kufanikisha kukamilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuwashukuru Katibu Mkuu Dr. Enos Bukuku na Naibu Katibu Mkuu, Bwana Omar Bendera,Wakurugenzi, Viongozi wa Asasi

na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji ambao wamefanya kazi kwa bidii na kufanikisha kukamilisha taarifa hii. Pia, napenda kuwashukuru viongozi na wafanyakazi wenzetu wa Wizara, Mikoa, Idara mbalimbali za Serikali, Mashirika ya Umma na Taasisi kwa ushikiano wao wakati wa kuandaa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki cha mwaka mmoja Wabunge wenzetu wanne ambao tulikuwa nao mwaka jana wakati kama huu, hatunao tena. Kwa masikitiko makubwa, naomba kutoa rambirambi kwa jamaa, ndugu na familia za Waheshimiwa Wabunge wote waliofariki. Wabunge hao ni Marehemu Theodos Kasapira - Mbunge wa Ulanga Mashariki, Marehemu Frank Mussati - Mbunge wa Kasulu Mashariki, Marehemu Balozi Ahmed Hassan Diria - Mbunge wa Rahaleo, Marehemu Abuu Kiwanga - Mbunge wa Kilombero. Tunamwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa mapitio ya malengo ya jumla ya uchumi, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza kwa dhati Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete - Mbunge na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa kuchaguliwa na Chama Cha Mapinduzi kuwa Mgombea wa Kiti cha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein - Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa kuwa Mgombea mwenza. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Amani Abeid Karume kwa kuchaguliwa na *CCM* kuwa Mgombea wa Urais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2005. Sote tuna hakika kwamba *CCM* itapata ushindi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mapitio ya malengo ya jumla ya uchumi, katika kipindi hiki, tumeshuhudia mageuzi ya kiuchumi na kijamii, kitaifa na kimataifa ambayo yamechangia kuleta mafanikio makubwa ya ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Mabadiliko makubwa katika maendeleo ya uchumi wa nchi yetu yameonekana hasa katika ukuaji wa pato la Taifa. Hali hii ya ukuaji wa uchumi wa nchi yetu iliimarika kutokana na hatua za kisera na kimkakati ambazo Serikali ilitayarisha na kusimamia utekelezaji wake.

Hatua hizo ni pamoja na kukamilisha maandalizi na kuanza kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 kwa kutumia mipango na mikakati ya muda wa kati ikijumuisha Mkakati wa Kupunguza Umaskini.

Pili, kutayarisha na kutekeleza hatua kwa hatua na kwa ufanisi mikakati ya kutengeneza uchumi mkuu pamoja na kuboresha mifumo na mikakati ya makusanyo ya mapato.

Tatu, kuboresha na kutekeleza kwa ufanisi sera na mikakati ya kudhibiti matumizi ya Serikali, ujazi wa fedha, kasi ya upandaji bei, pamoja na kuhakikisha ulipaji wa madeni ya nje na ndani hali ambayo imeiongezea nchi hadhi na kuaminika mbele ya wahisani pamoja na wawekezaji.

Nne, kuboresha na kuendeleza mazingira ya sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika harakati za kuleta maendeleo na kuimarisha uchumi wa soko.

Tano, kurekebisha na kubinafsisha Mashirika ya Umma hali ambayo imechangia katika kuongeza mapato pamoja na nafasi za ajira pamoja na kuipunguzia Serikali mzigo wa kutoa ruzuku ya kuendeshea Mashirika hayo.

Sita, kuweka mazingira bora ya uwekezaji kwa kuimarisha miundombinu, kurekebisha sheria na mifumo pamoja na kuimarisha shughuli za Kituo cha Uwekezaji Tanzania.

Saba, kuweka mazingira ya Utawala Bora na Uwajibikaji kwa kuhamasisha Umma kushiriki katika michakato ya kuandaa, kusimamia na kutathimini sera, mipango na mikakati ya kukuza uchumi na kuondoa umaskini pamoja na kupambana na rushwa; na

Mwisho, kutayarisha na kuanza kutekeleza Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini wa Tanzania *(MKUKUTA).*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kufanya mapitio ya hali ya uchumi na maendeleo yetu kwa ufupi kwa kipindi cha utawala wa Serikali ya Awamu ya Tatu pamoja na mapitio ya hali ya uchumi ya mwaka 2004.

Itakumbukwa kwamba michakato ya mipango na bajeti kwa kipindi hiki iliendelea kujikita zaidi katika kufanya mageuzi ya kiuchumi na kijamii yaliyolenga katika kukuza na kutengemaza uchumi, kwa kutekeleza Mkakati wa Kupunguza Umaskini ili kufikia malengo ya jumla ya Dira ya Taifa ya Maendeleo mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, malengo ya jumla ya uchumi kwa kipindi cha muda wa kati ya mwaka 2003/2004 - 2005/2006 yalikuwa kama ifuatavyo:-

(1) Pato la Taifa kukua kwa asilimia 6.6 mwaka 2004 na asilimia 7.0 mwaka 2005 (Ukuaji halisi ulikuwa asilimia 3.6 mwaka 1995);

(2) Kasi ya Upandaji bei kupungua hadi asilimia 4.0 Juni, 2004 (Mwaka 1995 kasi ya upandaji bei ilikuwa asilimia 27.4);

(3) Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) kudhitibiwa ili uwiane na malengo ya ukuaji wa uchumi na kasi ya upandaji bei;

(4) Mapato ya ndani ya Serikali kuongezeka na kufikia asilimia 13.5 ya Pato la Taifa mwaka 2004/2005 na asilimia 13.7 mwaka 2005/2006;na

(5) Mapato ya fedha za kigeni kuongezeka ili yaweze kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma toka nje kwa kipindi kisichopungua miezi mitano.

Mheshimiwa Spika, pato la Taifa katika mwaka 2004, lilikua kwa asilimia 6.7 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.7 mwaka 2003. Ukuaji huu ulizidi matarajio ya asilimia 6.3 kwa mwaka 2004. Ongezeko kubwa la ukuaji, lilichangiwa hasa na Sekta za Kilimo, Biashara, inayojumuisha Utalii, uuzaji wa jumla na rejareja pamoja na huduma nyinginezo, Mawasiliano na Uchukuzi pamoja na uzalishaji bidhaa viwandani. Uzalishaji viwandani umeendelea kuongezeka kutokana na urekebishaji na ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma. Ukuaji uliongezeka katika Sekta za Mawasiliano, uendeshaji wa Serikali na utawala, huduma za fedha, Bima na biashara. Sekta za Uzalishaji Viwandani na Ujenzi zilikua kwa viwango vya mwaka 2003. Ukuaji katika Sekta za Madini, Maji na Umeme ulishuka.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwaka 2004, wastani wa kasi ya upandaji bei ilipanda na kufikia asilimia 4.2 ikilinganishwa na asilimia 3.5 mwaka 2003 (kwa bei za mwaka 2001). Kuongezeka kwa kasi ya upandaji bei kulitokana na kupanda kwa bei ya bidhaa za mafuta ya petroli na chakula. Aidha, kupanda kwa gharama za usafirishaji na upungufu wa chakula kulikotokea mwishoni mwa mwaka 2003 na miezi ya mwanzo ya mwaka 2004, kulisababisha kupanda kwa bei ya chakula.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Awamu ya Tatu, mapato ya ndani yaliongezeka kutoka Shilingi bilioni 448.4 mwaka 1995/1996 kufikia Shilingi bilioni 1,459 mwaka 2003/2004. Ongezeko la wastani wa makusanyo kwa kila mwezi liliongezeka kutoka Shilingi bilioni 25 kwa mwezi mwaka 1995/1996, hadi Shilingi bilioni 121.6 kwa mwezi mwaka 2003/2004. Katika nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2004/2005, mapato ya ndani yalifikia Shilingi bilioni 870.1, ikilinganishwa na Shilingi bilioni 713.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2003/2004. Mapato hayo ni sawa na wastani wa Shilingi bilioni 145.0 kwa mwezi ikilinganishwa na wastani wa Shilingi bilioni 118.9 kwa mwezi katika kipindi kama hicho mwaka 2003/2004.

Hadi Machi 2005, mapato ya ndani yalikuwa Shilingi bilioni 1,314.5 (wastani wa Shilingi bilioni 146 kwa mwezi) ikilinganishwa na Shilingi bilioni 1,089.3 (wastani wa Shilingi bilioni 121 kwa mwezi) katika kipindi kama hicho mwaka 2003/2004. Mapato hayo ni zaidi ya makisio kwa asilimia 1.7. Kuongezeka kwa mapato kulitokana hasa na kuendelea kuimarika katika usimamizi na ukusanyaji kodi, hususan, Kodi ya Mapato na Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* kwa bidhaa za ndani na nje.

Mheshimiwa Spika, hadi Machi, 2005 matumizi yote yalifikia jumla ya Sh.2,429,269/= ikilinganishwa na makisio ya Sh.2,486,892/= sawa na upungufu wa Sh.57,623,000/= au asilimia 2.3. Kati ya matumizi hayo, Sh.1,560,067/= zilikuwa kwa matumizi ya kawaida na Sh.869,202,000/= kwa miradi ya maendeleo. Kati ya matumizi ya kawaida Sh.152,122,000/= zilitumika kwa ajili ya kulipa riba na madeni. Miradi mingi zaidi ya maendeleo ilifanikiwa kutekelezwa baada ya kuongezeka kwa upatikanaji wa fedha za ndani na nje.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka ulioishia Desemba 2004, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana *(M2)* uliongezeka hadi asilimia 19.2 ikilinganishwa na asilimia 14.1

Desemba, 2003, ambapo ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi *(M3)* uliongezeka hadi asilimia 19.3 kutoka asilimia 16.6 mwezi Desemba, 2003. Hata hivyo, ongezeko hili lilikuwa chini ya kiwango cha lengo la wigo wa asilimia 20-24 kwa *M2* na asilimia 20-23 kwa *M3* katika mwaka 2004/2005. Ongezeko hilo lilitokana na fedha zilizotolewa na wafadhili kusadia katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mikopo kwa sekta binafsi iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 30 mwaka 2004, ikilinganishwa na asilimia 43.2 kwa mwaka 2003. Sekta zilizokopa kwa kiasi kikubwa ni pamoja na Madini, Viwanda, Uzalishaji katika Kilimo na Biashara. Kupungua kwa kiwango cha ongezeko la mikopo kulitokana na viwango vya riba za mikopo kuendelea kuwa juu, wakopaji wakubwa kutokuongezeka na ukosefu wa dhamana za rehani kwa mikopo. Aidha, wastani wa viwango vya riba za mikopo ulipungua kidogo kutoka asilimia 14.5 mwaka 2003, hadi asilimia 14.0 mwaka 2004. Lengo ni kupunguza zaidi viwango vya riba za mikopo katika muda wa kati ili kuhamasisha na kuongeza idadi ya wakopaji.

Mheshimiwa Spika, thamani ya mauzo ya bidhaa nje iliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 1,129.2 mwaka 2003 hadi Dola milioni 1,333.5 mwaka 2004, sawa na ongezeko la asilimia 18.2. Ongezeko hilo lilichangiwa zaidi na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa zisizo asilia hasa dhahabu. Mwaka 2004, thamani ya mauzo ya bidhaa zisizo asilia iliongezeka kwa asilimia 14.6 na kufikia Dola milioni 1,042.2 kutoka Dola milioni 908.7 mwaka 2003. Ongezeko hili lilichangiwa kwa kiasi kikubwa na mauzo ya madini hasa dhahabu ambayo bei yake iliongezeka katika Soko la Dunia. Mauzo ya madini yamekuwa yakichangia sehemu kubwa ya mauzo nje na yameongezeka kufikia Dola milioni 686.5 mwaka 2004 kutoka Dola milioni 552.2 mwaka 2003. Bidhaa nyingine zilizochangia ongezeko ni bidhaa za viwandani, samaki na mazao ya samaki pamoja na bidhaa za mboga na maua.

Mheshimiwa Spika, thamani ya mauzo ya bidhaa asilia katika mwaka 2004, iliongezeka kwa asilimia 32.6 kutoka Dola milion 220.5 mwaka 2003, hadi Dola milioni 292.3 mwaka 2004. Mafanikio haya yalichangiwa na kuongezeka kwa kiasi cha mauzo ya pamba kwa asilimia 60.4, tumbaku kwa asilimia 44.3 na korosho kwa asilimia 62.9, hali nzuri ya hewa pamoja na kuongezeka kwa matumizi sahihi ya mbolea na madawa ya kuulia wadudu.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004, thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje *(f.o.b)* iliongezeka kwa asilimia 18.0 hadi Dola milioni 2,281.8, ikilinganishwa na Dola milioni 1,933.5 mwaka 2003. Kiasi cha uagizaji wa bidhaa kiliongezeka zaidi kuliko kile kilichouzwa nje na hivyo kuleta nakisi katika urari wa biashara ya bidhaa. Kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa za kukuza mitaji, bidhaa za kati na za matumizi ya kawaida kulichangia kuongezeka kwa thamani ya uagizaji wa bidhaa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, urari wa biashara ya bidhaa ulikuwa na nakisi ya Dola milioni 948.2 mwaka 2004, ikilinganishwa na nakisi ya Dola milioni 804.2 mwaka 2003. Nakisi katika urari wa huduma ilikuwa Dola milioni 135.2 mwaka 2004, ikilinganishwa na nakisi ya Dola milioni 83.0 mwaka 2003. Urari wa malipo yote ulikuwa na nakisi ya

Dola milioni 323.0 mwaka 2004, ikilinganishwa na ziada ya Dola millioni 69.9 mwaka 2003. Nakisi ya mwaka 2004, ilichangiwa na kuongezeka kwa gharama kubwa za usafirishaji wa bidhaa kutoka nje kulikosababishwa na kuongezeka kwa wastani wa bei za mafuta ya petroli katika Soko la Dunia.

Mheshimiwa Spika, thamani ya Shilingi imeendelea kubadilika kufuatana na hali ya soko. Thamani ya Shilingi ilipanda kidogo kutoka wastani wa shilingi 1,107.0 kwa dola ya Marekani mwishoni mwa mwezi Juni 2004, hadi wastani wa Shilingi 1,060.0 mwishoni mwa mwezi Desemba, 2004. Ongezeko la thamani ya Shilingi lilitokana hasa na matokeo ya uuzaji wa fedha za kigeni uliofanywa na Benki Kuu kwa Mabenki ya ndani katika soko la fedha za kigeni, kwa lengo la kudhibiti ukwasi. Mwaka 2004, thamani ya Shilingi ya Tanzania ilikuwa na wastani wa Sh. 1,089.6 kwa Dola moja ikilinganishwa na wastani wa Sh.1,038 mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, hadi Desemba, 2004, deni la Taifa lilifikia Dola milioni 9,219.3 ikilinganishwa na Dola milioni 8,793.2 Desemba 2003, sawa na ongezeko la asilimia 5.0. Katika deni hilo Dola milioni 928.3 ni deni la ndani sawa na asilimia 10.1 ya deni lote na Dola milioni 8,291.0 ni deni la nje. Deni la ndani lilitokana hasa na mauzo ya hawala na dhima za Hazina na dhamana nyingine za Serikali.

Ongezeko la deni la Taifa la nje kwa mwaka 2004, lilitokana na malimbikizo ya riba kwa madeni ambayo hayajasamehewa na kutolewa kwa mikopo mipya na wahisani, hususan Mashirika ya Kimataifa. Pamoja na kwamba nchi wahisani waliendelea kutoa misamaha ya deni la nje chini ya utaratibu wa Mpango wa Kuzipunguzia Madeni Nchi Maskini zenye madeni makubwa, mwenendo wa deni uliendelea kuzingatia mwelekeo na vigezo vya Mkakati wa Taifa wa Madeni.

Mheshimiwa Spika, pato la dunia lilikua kwa asilimia 5.1 mwaka 2004, ikilinganishwa na asilimia 4.0 mwaka 2003. Pato la nchi zilizoendelea lilikua kwa asilimia 3.4 mwaka 2004, ikilinganishwa na asilimia 2.0 mwaka 2003. Kwa upande wa nchi zinazoendelea, pato lilikua kwa asilimia 7.2 mwaka 2004, ikilinganishwa na asilimia 6.4 mwaka 2003. Pato la Afrika lilikua kwa asilimia 5.1 mwaka 2004, ikilinganishwa na asilimia 4.6 mwaka 2003, kiwango ambacho ni cha juu kabisa katika kipindi cha miaka kumi iliyopita.

Matukio ya kiuchumi na maendeleo yaliyochangia ukuaji wa uchumi Barani Afrika ni pamoja na kuimarika kwa uchumi duniani, misamaha ya madeni kwa nchi za Afrika, kuongezeka kwa uzalishaji katika Sekta ya Kilimo, kuimarika kwa bei za bidhaa asilia, pamoja na kutekeleza sera za kurekebisha uchumi. Hata hivyo, kiwango cha ukuaji wa pato la Afrika katika mwaka 2004 bado hakitoshi kuifikisha Afrika katika malengo ya kimataifa ya kupunguza umaskini kwa kiwango cha nusu ifikapo mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, pato la nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara lilikua kwa asilimia 5.1 mwaka 2004 ikilinganishwa na asilimia 4.2 mwaka 2003. Pato la nchi Kaskazini mwa Afrika lilikua kwa asilimia 4.9 mwaka 2004 ikilinganishwa na asilimia 6.1 mwaka 2003. Ukame ulioathiri shughuli za kilimo nchini Morocco ndiyo hasa

ulichangia kushuka kwa ukuaji wa pato hilo. Nchi za Pembe ya Afrika pato lake lilikua kwa asilimia 9.1 mwaka 2004, ikilinganishwa na asilimia 1.9 mwaka 2003. Ethiopia ilichangia sehemu kubwa ya ukuaji huo kwa pato lake kuongezeka kwa asilimia 11.6 mwaka 2004, baada ya kupungua kwa asilimia 3.9 mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, kwa nchi za Maziwa Makuu ikiwemo Tanzania pato lilikua kwa asilimia 5.4 mwaka 2004 ikilinganishwa na asilimia 4.1 mwaka 2003. Ukuaji huo ulichangiwa hasa na kuongezeka kwa uzalishaji katika Sekta ya Kilimo. Kwa upande wa nchi za Afrika ya Kati na Magharibi, pato lilikuwa kwa asilimia 5.6 mwaka 2004, ikilinganishwa na asilimia 7.2 mwaka 2003. Upungufu wa ukuaji huo ulisababishwa hasa na migogoro na machafuko ya kisiasa na vita nchini *Ivory Coast* na Sudani.

Mheshimiwa Spika, ni vyema takwimu hizi zikalinganishwa na ukuaji wa pato la Taifa la Tanzania la asilimia 6.7 mwaka 2004 ili tujielewe wapi tunaposimamia kimaendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka 10 iliyopita, uhusiano wa nchi yetu na Mataifa mengine duniani pamoja na Mashirika ya Kimataifa na ushirikiano wa kikanda umeimarika kwa kiwango kikubwa na hivyo kulijengea Taifa mazingira mazuri kwa shughuli za kiuchumi. Pia, nchi yetu imeendelea kushiriki katika shughuli mbalimbali za maendeleo za kikanda kwa lengo la kuunganisha nguvu ili kuwa na sauti ya pamoja katika kudai mfumo wa kimataifa wenye maslahi sawa kwa nchi zote.

Mheshimiwa Spika, baada ya majadiliano kukamilika juu ya utaratibu wa kuondoleana ushuru, kuthibitisha uasili wa bidhaa na wigo wa pamoja wa ushuru wa forodha kwa bidhaa mbalimbali, Wakuu wa nchi za Tanzania, Uganda na Kenya walitia saini Itifaki ya Ushuru wa Pamoja tarehe 2 Machi, 2004. Pia, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania liliridhia Itifaki hiyo kwa kuungana na Mabunge ya Uganda na Kenya. Itifaki ilianza kutekelezwa tarehe 1 Januari, 2005.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majukumu mengine muhimu yanayotekelezwa na *SADC*, Mkakati wa Kupunguza na Kumaliza Matatizo Yanayohusiana na Siasa, Ulinzi na Usalama *(Strategic Indicative Plan for the Organ on Politics, Defence and Security (SIPO))* ulizinduliwa rasmi Agosti, 2004. Lengo la mkakati huo ni kuharakisha utekelezaji wa Mkakati wa Mpango wa Maendeleo wa Ushirikiano *(Regional Indicative Strategic Development Plan)* uliozinduliwa Machi, 2004.

Mheshimiwa Spika, Mpango Mpya wa Ushirikiano ili Kuleta Maendeleo Afrika *(NEPAD)*. Mwaka 2004, maandalizi ya utekelezaji wa Mkakati Mpana wa Kuendeleza Kilimo Afrika yalianza. Benki ya Dunia ilitoa Dola milioni 500 katika kuanzisha Programu ya Mkakati huo. Aidha, katika kufanikisha Mpango wa Utekelezaji wa Muda Mfupi kuhusu Miundombinu, Benki ya Maendeleo ya Afrika ilikubali kufadhili miradi ya uwekezaji inayogharimu Dola milioni 580 na Benki ya Dunia iliidhinisha miradi inayogharimu Dola milioni 570.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ilitia saini Mkataba wa kujiunga na utaratibu unaotoa fursa kwa nchi kujitathmini na kujipima zenyewe *(African Peer Review Mechanism - APRM)* kuhusiana na utekelezaji wa vigezo muhimu vya *NEPAD* kwenye Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika Julai, 2004. Nchi 14 zilijiunga na utaratibu wa *APRM* katika mwaka huo na kufanya nchi zilizojiunga kufikia 23.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya mapendekezo ya Tume ya Kimataifa kuhusu Masuala ya Kijamii katika Utandawazi iliwasilishwa katika Kikao maalumu cha Shirika la Kazi Duniani mnamo mwezi Juni, 2004. Aidha, mapendekezo hayo na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC),* Umoja wa Afrika *(AU)* na Umoja wa Mataifa *(UN).* Matokeo yake ni kukubaliwa kuanza kwa utekelezaji wa taarifa hii ambapo Tanzania na Burkina Faso zimeteuliwa kutekeleza mapendekezo ya Tume kwa majaribio.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Tanzania, imeanza kutekeleza mapendekezo ya Tume kwa kuunda Kamati ya Kitaifa ya Utandawazi inayounganisha Sekta mbalimbali za Serikali, Asasi na Taasisi za Elimu ya Juu na zile za Utafiti chini ya Uenyekiti wa Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, hapo mwishoni mwa mwaka 2004. Kamati hii imechambua mapendekezo ya Tume na kuandaa mpango wa utekelezaji wa muda wa kati na muda mrefu. Mpango huu unaendelea kujadiliwa na Serikali pamoja na Shirika la Kazi Duniani. Vilevile, Kamati imetafsiri kwa lugha ya Kiswahili muhtasari wa Ripoti ya Tume ili iweze kueleweka vizuri kwa walengwa wengi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 1995 hadi 2004, Sekta ya Kilimo imeendelea kutoa mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi kwa kuchangia wastani wa asilimia 48.8 ya pato la Taifa, asilimia 66 ya mapato ya fedha za kigeni na kutoa ajira kwa asilimia 70 ya Watanzania. Kutokana na utekelezaji wa sera na mikakati ya kuendeleza kilimo, kilimo kilikuwa kutoka asilimia 3.4 mwaka 2000 hadi asilimia 6.0 mwaka 2004 ikilinganishwa na asilimia 4.0 mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa mazao ya chakula uliongezeka kutoka tani 11,979,000 mwaka 2003 hadi tani 13,213,000 mwaka 2004 sawa na ongezeko la asilimia 10.3. Hali hiyo ilichangiwa hasa na ongezeko la uzalishaji katika mazao ya mahindi, maharage na mpunga.

Uzalishaji wa mazao ya biashara uliongezeka kufikia tani 829,994 mwaka 2004 kutoka tani 603,840.6 mwaka 2003 sawa na ongezeko la asilimia 37.5. Ongezeko hilo lilichangiwa hasa na ukuaji katika uzalishaji wa mazao ya pamba, tumbaku na sukari. Mazao ya pareto yalipungua uzalishaji wake kwa asilimia 70.1 na hii ilitokana na wakulima kuacha kulima zao hilo kutokana na kukosekana kwa soko.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004 hekta 227,486 zilikuwa zimeendelezwa kwa kilimo cha umwagiliaji ikilinganishwa na eneo lililoendelezwa mwaka 2003 la hekta 216,244 sawa na ongezeko la asilimia 5.2. Hali hiyo imeongeza uzalishaji wa mpunga kwenye maeneo ya umwagiliaji maji kutoka tani 821,051 mwaka 2003, hadi tani 863,736 mwaka 2004.

Upatikanaji wa mbegu bora za mazao ya nafaka, mikunde na mbegu za mafuta umeongezeka kutoka tani 2,750 mwaka 1995/1996 hadi tani 10,650 mwaka 2003/2004. Vilevile, katika mwaka 2003/2004 Serikali ilirejesha utaratibu wa utoaji ruzuku ya mbolea kwa Mikoa ya Nyanda za Juu na hivyo kuongezeka kwa bajeti ya ruzuku ya mbolea kutoka Shilingi bilioni 2.0 mwaka 2002/2003 kufikia Shilingi bilioni 7.244 mwaka 2004/2005. Aidha, Vituo vya Kusambaza Mbolea vimeongezeka kutoka vitano mwaka 2003 hadi Vituo 13 mwaka 2004

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa nyama uliongezeka kutoka tani 341,500 mwaka 2003 hadi tani 348,800 mwaka 2004 sawa na ongezeko la asilimia 2.1. Uzalishaji wa maziwa uliongezeka kutoka lita 980,500 mwaka 2003 hadi lita 1,180,000 mwaka 2004. Uzalishaji wa ngozi uliongezeka kutoka vipande milioni 1.3 mwaka 2000 hadi vipande 1.6 mwaka 2004 sawa na ongezeko la asilimia 23. Ongezeko katika zao la ngozi limetokana na Serikali kuanzisha Mfuko wa Kuinua Sekta Ndogo ya Ngozi, pamoja na kutoa elimu kwa wafugaji na wachungaji kuhusu mchakato mzima wa utunzaji wa mazao ya ngozi ili kupata bei nzuri.

Mheshimiwa Spika, kwa Sekta ya Kilimo na Mifugo katika mwaka 2005/2006, juhudi zitaelekezwa katika kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji, kuboresha huduma za ugani, uzalishaji na matumizi ya mbegu bora pamoja na kuweka mazingira bora zaidi kwa ajili ya ushiriki wa sekta binafsi katika uzalishaji, usindikaji, usafirishaji na usambazaji wa mazao na pembejeo za kilimo. Vilevile, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi itaendelea kuhamasisha na kushiriki katika kazi za uchimbaji wa malambo na majosho, pamoja na shughuli za kuboresha afya za mifugo. Serikali itaendelea na hatua za kutoa vivutio kwa Sekta ya Mifugo ili iweze kutoa mchango mkubwa kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004, Sekta ya Viwanda ilikua kwa kiwango sawa na kile cha mwaka 2003 cha asilimia 8.6. Ukuaji huu ulitokana na utekelezaji wa programu mbalimbali ikiwemo Sera ya Ubinafsishaji, ambapo viwanda vingi vilipata wawekezaji wenye uwezo na uzoefu wa kuviendesha. Vilevile, Sera ya Uwekezaji imekuwa kivutio kwa wawekezaji wapya kuhamasika kuanzisha viwanda vipya hasa katika maeneo ya usindikaji wa mazao ya chakula, mbegu za mafuta ya kula, chai, sukari, usindikaji wa matunda, usagishaji wa nafaka, bidhaa za mbao, viwanda vya bidhaa za chuma na vifaa vya ujenzi.

Aidha, katika kutekeleza programu za Sera ya Viwanda Vidogo na vya kati wananchi wengi zaidi wameanza kuhamasika kuanzisha viwanda vidogo, hivyo kutoa mchango katika juhudi za kupunguza umaskini kwa njia ya kuongeza bidhaa zinazozalishwa, nafasi za ajira pamoja na mapato yao.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, mkazo utawekwa katika kuanzisha na kuimarisha uzalishaji katika Sekta ya Viwanda, hasa viwanda vidogo na vya kati kwa lengo la kuongeza ubora wa bidhaa, mapato, nafasi za ajira pamoja na kuanzisha maeneo maalum ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004, Sekta ya Madini ilikua kwa asilimia 15.6 ikilinganishwa na asilimia 18 mwaka 2003. Sababu kubwa ya kushuka kwa ukuaji huu ni kutokana na shughuli kubwa za uwekezaji katika miradi mikubwa ya uchimbaji madini kukamilika. Aidha, mchango wa Sekta ya Madini katika pato la Taifa uliongezeka kutoka asilimia 3.0 mwaka 2003, hadi asilimia 3.2 mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, takwimu za mwaka 2004, zimeonyesha kwamba thamani ya madini yaliyouzwa katika soko la nchi za nje ilifikia Dola milioni 686.5 ikilinganishwa na Dola milioni 552.2 mwaka 2003. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 19.6. Mojawapo ya sababu za ongezeko hili ni kuongezeka kwa upatikanaji wa madini ya almasi pamoja na bei nzuri ya dhahabu katika soko la nje.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2005/2006, Serikali itaendelea kuboresha uhusiano kati ya wachimbaji wadogo na wachimbaji wakubwa ili waweze kutoa mchango wao katika kuendeleza Sekta ya Madini. Aidha, shughuli za uchimbaji zitaboreshwa ili ziweze kufanyika kwa usalama na kuzingatia hifadhi ya mazingira. Vilevile, juhudi za makusudi zitafanyika kuanzisha viwanda vya kukata na kusanifu vito.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka 10 iliyopita, Serikali imepata mafanikio makubwa katika ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara kuu za Mikoa na Vijijini. Mafanikio haya yametokana na kuanzishwa kwa Bodi na Mfuko wa Barabara mwaka 1999, pamoja na Wakala wa Barabara mwaka 2000. Hadi mwaka 2004, mtandao wa barabara za lami zenye urefu wa Kilometa 4,837 na za changarawe/udongo zenye urefu wa Kilometa 80,063 zimejengwa ambapo mwaka 1995 kulikuwa na Kilometa 3,880 za lami na Kilometa 81,420 za changarawe/udongo nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hadi mwaka 2004, hali ya mawasiliano ya barabara Vijijini iliendelea kuimarika kutokana na kuzifanyia matengenezo ya kawaida, kuboresha sehemu korofi, pamoja na kukarabati makaravati na madaraja mbalimbali. Kazi hiyo ilisimamiwa na Halmashauri za Wilaya. Hali hiyo imeboresha zaidi usafiri wa watu pamoja na usafirishaji bidhaa.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2005/2006, Mkazo mkubwa utaendelea kuelekezwa kwenye barabara za Mikoa na barabara muhimu Vijijini zinazokwenda kwenye maeneo ya uzalishaji ili kukuza uchumi na kupunguza umaskini nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004, Sekta ya Mawasiliano na Uchukuzi ilikua kwa kiwango cha asilimia 6.2 ikilinganishwa na asilimia 5.0 mwaka 2003. Mchango wa sekta katika pato la Taifa umeendelea kuwa asilimia 5.4 sawa na kiwango cha mwaka 2003. Ukuaji wa Sekta umechangiwa na ongezeko kubwa la wateja wa simu za mkononi na kuimarika kwa barabara nyingi ambako kumerahisisha uchukuzi wa shehena za mizigo hususan mazao ya kilimo na viwanda, malighafi na kuimarika kwa huduma za Posta.

Mheshimiwa Spika, mafanikio yameendelea kuonekana kwenye huduma za usafiri wa anga na majini, huduma za Mamlaka ya Bandari Tanzania hasa Kitengo cha Makontena utendaji wake uliendelea kuboreshwa na kuongeza tija.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004, Sekta Ndogo ya Mawasiliano hasa upande wa simu za mkononi, iliendeshwa kwa ufanisi. Wateja wa simu za mkononi waliongezeka kutoka 1,298,000 mwaka 2003 hadi 1,788,749 mwaka 2004 sawa na ongezeko la asilimia 37.8. Aidha, huduma za Posta nazo ziliimarika hasa upande wa usafirishaji wa barua za ndani na nje, fedha na utumaji ujumbe kwa njia ya haraka.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha udhibiti katika Sekta ya Mawasiliano na Uchukuzi, Mamlaka ya Udhibiti wa Usafirishaji wa Nchi Kavu na Majini *(SUMATRA)* pamoja na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Anga zilianzishwa na kuanza shughuli zake rasmi mwaka 2004. Uanzishwaji wa Mamlaka hizi utasaidia sana katika udhibiti na ufuatiliaji wa shughuli za Sekta ya Mawasiliano na Uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Serikali itaendelea na juhudi zake za kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Aidha, juhudi za kuhimiza matumizi ya teknolojia sahihi zitaendelezwa ili huduma za mawasiliano na uchukuzi zifanyike kwa ubora na ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004, Sekta ya Nishati ilikua kwa asilimia 4.9 ikilinganishwa na asilimia 5.0 mwaka 2003. Kushuka kwa ukuaji wa Sekta hii kumetokana hasa na ukame ambao ulisababisha upungufu mkubwa wa uzalishaji umeme unaotokana na nguvu za maji na kupanda kwa bei ya mafuta kwenye Soko la Dunia. Kutokana na hali hiyo, umeme uliozalishwa nchini ulipungua kutoka *Gigawatt 2,661.7* mwaka 2003 hadi *Gigawatt 2,126.4* mwaka 2004, sawa na upungufu wa asilimia 20.

Kwa upande wa matumizi ya petroli, jumla ya mita za ujazo milioni 1.45 zilitumika mwaka 2004, ikilinganishwa na mita za ujazo milioni 1.35 mwaka 2003. Mchango wa Sekta ya Nishati katika pato la Taifa mwaka 2004, ulikuwa sawa na ule wa mwaka 2003 wa asilimia 1.4.

Mheshimiwa Spika, Serikali ikishirikiana na wadau mbalimbali imekamilisha ujenzi wa mradi wa gesi ya Songosongo ikiwa ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa bomba kutoka Kisiwa cha Somanga hadi Ubungo Julai, 2004. Gesi hii imeanza kutumiwa na baadhi ya viwanda kwa ajili ya kuendeshea mitambo katika Mkoa wa Dar es Salaam. Baadhi ya viwanda hivyo ni:-

Kiwanda cha Sementi -Wazo, Kiwanda cha Bia -*TBL*, Kiwanda cha Bora na Kiwanda cha Kioo. Kwa upande wa gesi asilia ya mradi wa *Mnazi Bay* maandalizi yanaendelea vizuri. Tayari vifaa na zana mbalimbali zimepelekwa katika eneo hilo na kuhifadhiwa Msimbati. Timu ya wataalam pia imepelekwa kuhakiki michoro inayoonyesha vyanzo vya gesi katika maeneo hayo ili Mradi uanze rasmi.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza azma yake ya kupeleka umeme Vijijini ili kuharakisha maendeleo na kupunguza umaskini, mwezi Aprili, 2004, Serikali imepitisha

Muswada wa kuanzisha Wakala wa Nishati Vijijini *(Rural Energy Agency–REA)* na Mfuko wa Nishati Vijijini *(Rural Energy Fund – REF).*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Serikali itaendelea na juhudi za kukuza, kuboresha na kusambaza huduma za umeme Mijini na Vijijini. Vilevile, mikakati inayolenga katika kuongeza ufanisi na kuruhusu ushindani katika Sekta ya Nishati, pamoja na kuimarisha na kuendeleza juhudi za tafiti za nishati nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuhamasisha Serikali za Mitaa na wadau wengine katika kuanzisha madarasa ya Elimu ya Awali katika kila Shule ya Msingi. Kutokana na mwitikio, idadi ya wanafunzi wa madarasa ya Elimu ya Awali imeongezeka kutoka 554,635 mwaka 1995, hadi 960,470 mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 1995 hadi 2004, jumla ya madarasa 84,184, nyumba za walimu 20,955 na matundu ya vyoo 159,232 yalijengwa pamoja na kununua madawati 1,480,512. Pia, idadi ya walimu iliongezeka kutoka 105,280 mwaka 1995, hadi 145,295 mwaka 2004. Aidha, kiwango cha jumla cha uandikishaji *(GER)* kimeongezeka kutoka asilimia 77.5 mwaka 1995, hadi 106.3 mwaka 2004. Kiwango halisi cha uandikishaji kimeongezeka kutoka asilimia 55.3 mwaka 1995, hadi 90.5 mwaka 2004. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamekuwepo na ongezeko la kuridhisha la idadi ya wanafunzi wanaojiunga na Elimu ya Sekondari. Mwaka 1995 kulikuwa na wanafunzi wa Kidato cha Kwanza mpaka cha Sita 196,375 na mwaka 2004 walifikia 432,599 likiwa sawa na ongezeko la asilimia 120.3. Aidha, katika mwaka 1995 uwiano wa wasichana kwa wavulana ulikuwa 44.4 kwa 55.6 ikilinganishwa na uwiano wa 46.2 kwa 53.8 mwaka 2004. Vilevile, kiwango cha wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na Elimu ya Sekodari (Kidato cha Kwanza) kimeongezeka kutoka asilimia 14.6 mwaka 1995 hadi asilimia 30.1 mwaka 2003. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imepata mafanikio katika maeneo mbalimbali ya Elimu ya Juu yakiwemo, ushirikishwaji wa sekta binafsi katika kutoa Elimu ya Juu, kuboresha mazingira ya ufundishaji pamoja na urekebishaji wa mitaala ili iendane na mahitaji ya soko la ajira. Idadi ya wanafunzi waliojiunga na Vyuo vya Ufundi vya Umma imeongezeka kutoka 1,896 mwaka 1995/1996, hadi 2,103 mwaka 2003/2004 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 11. Katika kipindi hicho, idadi ya wanafunzi wa kike waliojiunga iliongezeka kwa asilimia 109. Aidha, idadi ya waliojiunga na Vyuo vya Umma vya Elimu ya Juu imeongezeka kutoka 7,785 mwaka 1995/1996, hadi 28,910 mwaka 2003/2004, ikiwa ni ongezeko la asilimia 271.0. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mafanikio yaliyopatikana hadi sasa katika Shule za Msingi chini ya Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi *(MMEM),* katika mwaka 2005/2006, Serikali itaendelea na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari *(MMES)* kwa lengo la kuipanua na kuiboresha ili kukabiliana na ongezeko la idadi ya wanafunzi wanaohitimu Elimu ya Msingi. Vilevile, Serikali

itaendelea kuboresha zaidi mazingira ya kutoa elimu, uwiano wa kijinsia, kuimarisha mfumo wa habari, elimu, mawasiliano, pamoja na mfumo wa uongozi katika ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, kuendelea kutekelezwa kwa Sera ya Maji ambayo inasisitiza wananchi kushirikishwa zaidi katika Miradi ya Maji na usimamizi wake, kumesaidia kuongezeka kwa usambazaji wa maji katika maeneo ya Vijijini hadi asilimia 53.5 mwaka 2004, kutoka asilimia 53.0 mwaka 2003. Aidha, idadi ya watu waliopata huduma ya maji safi iliongezeka kutoka 13,825,161 mwaka 2003 hadi 14,553,853 mwaka 2004. Katika maeneo ya Mijini kwa mwaka 2004 huduma za usambazaji maji zimeendelea kuwa asilimia 74, kama zilivyokuwa mwaka 2003 kutokana na ongezeko la watu Mijini. Uondoaji wa maji taka Mijini umeongezeka kutoka asilimia 10 mwaka 2003 hadi asilimia 17 mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Serikali itaendelea na juhudi za kuongeza na kuboresha huduma za usambazaji maji kwa lengo la kuongeza idadi ya watu wanaopata huduma ya maji Mijini na Vijijini, kulinda vyanzo vya maji na mazingira pamoja na kuongeza upatikanaji wa maji kwa kuvuna maji ya mvua. Aidha, Serikali itahamasisha zaidi uanzishwaji wa Kamati na Mifuko ya Maji na vyombo vingine kwa lengo la kuboresha huduma za maji.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Afya, Hospitali zimeongezeka kutoka 194 mwaka 1995, hadi 233 mwaka 2004. Pia, Vituo vya Afya vimeongezeka kutoka 343 mwaka 1995, hadi 433 mwaka 2004 na Zahanati kutoka 3,832 hadi 4,622 kwa kipindi hicho. Pia, kumekuwepo na kuimarika kwa chanjo kutoka asilimia 30 mwaka 1995 hadi asilimia 89.4 mwaka 2004 katika kila Wilaya. Vilevile, Serikali imeendelea na udhibiti wa ugonjwa wa malaria ambapo imeendelea na kufanya utafiti wa ubora wa dawa. Aidha, idadi ya wanawake wanaotumia huduma za Kliniki imeongezeka kutoka asilima 70 mwaka 1995, hadi 90 mwaka 2004. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mojawapo ya lengo la Sekta ya Afya ni kupunguza vifo vya watoto walio na umri chini ya miaka mitano kutoka watoto 158 kwa kila watoto 1000 waliozaliwa hai mwaka 1999 hadi watoto 127 mwaka 2003. Takwimu za Sensa zinaonyesha kwamba mwaka 2002, idadi ya vifo vya watoto chini ya umri wa miaka mitano ilipungua hadi watoto 154 kwa kila watoto 1000 waliozaliwa hai. Juhudi zaidi za kupunguza vifo vya watoto chini ya umri wa miaka mitano zinakwamishwa na kuendelea kuongezeka kwa watoto wanaozaliwa wakiwa wameathirika na virusi vya *UKIMWI*, kuongezeka kwa idadi ya watoto yatima na kuongezeka kwa malaria.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Serikali itaendelea kuboresha Sekta ya Afya kwa kutenga fedha zaidi kwa ajili ya kuhakikisha kwamba madawa muhimu yakiwemo ya kurefusha maisha kwa walioathirika na *UKIMWI* yanapatikana; kuhakikisha utekelezaji wa mipango na mikakati mbalimbali ya afya ya jamii na ya msingi ukiwemo Mkakati ya Kutibu Magonjwa ya Watoto kwa Uwiano; kuboresha huduma za kudhibiti maambukizi ya magonjwa hasa kifua kikuu na ukoma na kufanya kampeni za kutokomeza surua pamoja na kuimarisha utafiti katika Sekta ya Afya.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki, Serikali ilifanya maamuzi ya kisera yanayogusa Sekta zote yakiwa yameelekezwa katika harakati za kukuza uchumi na kuondoa umasikini. Maamuzi hayo ni pamoja na Urekebishaji na Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka kumi iliyopita Serikali iliendelea na urekebishaji na ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma. Hadi Desemba, 2004 jumla ya Mashirika 312 yamebinafsishwa na mali za Mashirika zipatazo 499 zimeuzwa ikilinganishwa na Mashirika 289 na mali za Mashirika zipatazo 328 hadi mwaka 2003. Katika zoezi hilo Watanzania wengi wamepata fursa ya kuwa wawekezaji. Mchanganuo wa umiliki wa Mashirika haya 312 yaliyobinafsishwa, unaonyesha kuwa Mashirika 160 yamenunuliwa na Watanzania kwa asilimia 100, Mashirika 24 yamenunuliwa na wawekezaji wa nje kwa asilimia 100 na Mashirika 128 yamenunuliwa kwa ubia baina ya wawekezaji Watanzania na wa nje.

Mheshimiwa Spika, ubinafsishaji umetuletea mafanikio ikiwa ni pamoja na kuiondolea Serikali mzigo wa kutoa ruzuku kwa Mashirika ya kibiashara na kuyawezesha kuchangia ipasavyo katika pato la Taifa.  Aidha, teknolojia na mitaji ya kisasa imeingizwa nchini na kuongeza ajira kwa Watanzania.  Pia, sekta isiyo rasmi imepanuka kwa kuwawezesha wananchi kufanya biashara na Mashirika yaliyobinafsishwa.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na kuanzishwa kwa Mamlaka za Udhibiti na kufanya marekebisho ya sheria za Sekta zinazolenga kudhibitiwa na mamlaka hizo. Mamlaka zilizoundwa na kuanza kufanya kazi ni Mamlaka ya Udhibiti ya Mawasiliano *(TCRA)*, Mamlaka ya Udhibiti ya Usafirishaji wa Majini na Nchi Kavu *(SUMATRA),* na Mamlaka ya Udhibiti ya Mawasiliano ya Anga *(TCAA).*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005/06, Serikali itaendelea kwa makini kubinafsisha Mashirika ya Umma ambayo yameainishwa kwa ajili ya zoezi hilo yakiwemo *NMB*, Vitengo vya kibiashara vya *THA* vilivyosalia, *TANESCO, TAZARA, NIC, TRC*, Viwanda vya Korosho, Mashamba ya *NAFCO* na *NARCO*.  Vilevile, Serikali itaendelea kuimarisha vitengo vya usimamizi, ufuatiliaji na tathmini ya Mashirika yaliyobinafsishwa kwa lengo la kuboresha utendaji wake.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya juhudi kubwa ya kuvutia wawekezaji wa ndani na wa nje ya nchi kwa kuweka mazingira mazuri ya kibiashara. Kutokana na juhudi hizo kuanzia mwaka 1995, hadi Desemba 2004, Kituo cha Uwekezaji Tanzania kiliidhinisha miradi 2,321 yenye thamani ya Sh.7, 587,078/= na inakadiriwa kutoa nafasi za ajira 447,290 hadi mwaka 2004. Katika mwaka 2004, Kituo cha Uwekezaji kilisajili jumla ya miradi 454 yenye thamani ya Sh. 1,246,040/= sawa na Dola bilioni 1.26.

Kati ya miradi hiyo, miradi 269 ilikuwa mipya na miradi 185 ilikuwa ya kupanua na kukarabati viwanda.  Miradi 208 ilikuwa ya wawekezaji wa ndani, 119 wawekezaji wa nje na 127 ilikuwa ya ubia. Vilevile, uwekezaji mitaji wa moja kwa moja kutoka nje uliongezeka toka Dola milioni 247.8 mwaka 2003, hadi Dola milioni 260.2 mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Serikali itaendelea kuhimiza wawekezaji wa ndani kuwekeza katika viwanda vidogo na vya kati vya kusindika mazao ili kuongeza thamani ya mauzo nje na kuchangia katika kupanua nafasi za ajira. Hali kadhalika, Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuboresha Kituo cha Uwekezaji na kuendeleza uwekezaji katika sekta mbalimbali za kiuchumi, pamoja na kuboresha mazingira ya biashara pamoja na uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya utafiti uliofanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Kudhibiti *UKIMWI* Tanzania Bara, mwaka 2003/2004 katika ngazi ya kaya, yameonyesha kwamba wastani wa asilimia 7.0 ya Watanzania wenye umri wa miaka 15 hadi 49 wameambukizwa virusi vya *UKIMWI*. Utafiti huo pia ulionyesha kuwa kiwango cha maambukizi ni kikubwa kwa wanawake kuliko wanaume, ambapo asilimia 7.7 ya wanawake wana maambukizi ya *UKIMWI* ikilinganishwa na asilimia 6.3 ya wanaume. Pia, imeonekana kwamba *UKIMWI* umeenea zaidi katika maeneo ya Mijini ambapo asilimia 10.9 ya wakazi wa maeneo hayo wameambukizwa *UKIMWI* ikilinganishwa na asilimia 5.3 ya wakazi wa Vijijini.

Mheshimiwa Spika, utafiti pia umebaini kuwa hali ya maambukizi inazidi kutofautiana kati ya Mikoa. Mikoa ya Mbeya, Iringa na Dar es Salaam imekuwa na viwango vya juu vya maambukizi karibu mara mbili ya wastani wa Watanzania wote wenye umri wa miaka kati ya 15 - 49. Utafiti umeonyesha kuwa Mikoa ya Manyara na Kigoma ina viwango vya chini vya maambukizi ambayo ni wastani wa asilimia 2.0. Katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Serikali itaendelea na kutekeleza Mkakati wa Kudhibiti *UKIMWI* pamoja na kuwezesha upatikanaji na matumizi ya madawa ya kurefusha maisha kwa watu waishio na Virusi vya *UKIMWI* katika kila Mkoa.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya Ulingo wa Beijing inaonyesha kuwa Tanzania imepata mafanikio makubwa katika kuingiza masuala ya jinsia katika Sera, Programu, Mipango na Mikakati mbalimbali ya Taifa. Kutokana na marekebisho yaliyofanywa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ongezeko la uwakilishi wa wanawake katika ngazi mbalimbali za maamuzi limepatikana. Kutokana na marekebisho hayo, kumekuwepo na ongezeko la Wabunge wanawake kutoka asilimia 17.5 mwaka 1995, hadi asilimia 22.5 mwaka 2004. Sheria za uchaguzi zinaendelea kurekebishwa ili kuwa na uwakilishi wa Wabunge wanawake unaofikia asilimia 30. Vilevile, uwakilishi katika ngazi ya Serikali za Mitaa kwa upande wa wanawake umeongezeka kutoka asilimia 25 mwaka 1995, hadi asilimia 33.3 mwaka 2004. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, yapo mafanikio makubwa katika kuwawezesha wanawake kwa kupata nafasi katika ngazi mbalimbali za uongozi. Katika mwaka 2004, Idadi ya Makatibu tawala wanawake iliongezeka kufikia 5 ikilinganishwa na 4 mwaka 2003. Idadi ya Wakuu wa Wilaya wanawake iliongezeka toka 19 mwaka 2003 hadi kufikia 23 mwaka 2004. Kulikuwa na ongezeko kubwa la Wakurugenzi wa Wilaya mwaka 2004 kufikia 23 toka 14 mwaka 2003. Mwaka 2004, idadi ya Makatibu Wakuu wanawake iliongezeka kufikia 7 kutoka 6. Pia kulikuwa na ongezeko la Wakurugenzi katika Idara za Serikali kutoka 29 mwaka 2003 kufikia 30 2004. Vile vile, idadi ya Majaji wanawake ilifikia 7 mwaka 2004 kutoka Majaji 6 mwaka 2003. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeendelea kufanya marekebisho na utekelezaji wa Sheria za Makosa ya Kujamiiana na ya Ardhi na Sheria ya Vijiji ya Mwaka 1999, katika kuhakikisha kwamba haki za wanawake zinalindwa. Aidha, kuanzishwa kwa Vitengo vya Jinsia katika Wizara na Taasisi za Serikali kutaharakisha kasi ya kuingiza masuala ya jinsia kwenye mipango na mikakati hatua kwa hatua katika ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Serikali itaendelea kuboresha sera, mipango na mikakati ili iweze kuzingatia masuala ya jinsia na kuhamasisha matumizi ya takwimu zilizochambuliwa kijinsia katika maamuzi mbalimbali. Serikali itahakikisha kiwango cha uwakilishi wa wanawake katika ngazi zote kinazingatiwa pamoja na kuhakikisha kuwa wanawake wanapewa fursa ya kujiendeleza kielimu na kiuchumi ili waweze kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza juhudi za kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Serikali imetayarisha na kutekeleza sera, miongozo na mikakati mbalimbali. Katika kipindi cha mwaka 2000/2001-2002/2003, Serikali iliandaa na kutekeleza Mkakati wa Kupunguza Umaskini. Mipango mingine iliyotayarishwa ni pamoja na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania *(MKUKUTA),* Mkakati wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania *(MKURABITA),* Mpango wa Kuendeleza Sekta Binafsi, Mpango Maalum wa Kuharakisha Maendeleo Tanzania na Mpango wa Muda wa Kati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini ambao ulikuwa wa miaka mitatu unafanyiwa marekebisho ili kuainisha utekelezaji wa malengo ya Dira 2025, kwa vipindi vya miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, Mkakati wa Kupunguza Umaskini ulitoa kipaumbele katika Sekta za Kilimo, Barabara za Vijijini, Maji, Afya, *UKIMWI*, Utawala Bora na Jinsia. Utekelezaji wake umeonyesha mafanikio katika Sekta mbalimbali kama yalivyoelezwa hapo awali. Aidha, utekelezaji wake umetoa changamoto na mafunzo yafuatayo:-

(i) Mafanikio yake hayakuweza kukidhi matarajio ya kufikia malengo ya programu mbalimbali za maendeleo ambazo hazikuwa kwenye Sekta za kipaumbele;

(ii) Utekelezaji wa Mkakati wa Kupunguza Umaskini haukuweza kufanikisha kikamilifu ukuaji endelevu wa uchumi;

(iii) Mkakati wa Kupunguza Umaskini haukuweza kuoanisha mikakati ya Sekta mbalimbali na malengo ya kupunguza umaskini;

(iv) Mkakati wa Kupunguza Umaskini uliimarisha uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa rasilimali za Umma zilizotolewa kwa ajili ya kutekeleza mipango ya kupunguza umaskini;

(v) Umeonyesha umuhimu wa kuoanisha Sera za Kitaifa na mgao wa rasilimali; na

(vi) Mkakati wa Kupunguza Umaskini umetoa msukumo katika kutekeleza Sera ya Serikali ya kupeleka fedha zaidi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, changamoto na mafunzo yaliyojitokeza katika kuandaa na kutekeleza Mkakati wa Kupunguza Umaskini, yalikuwa msingi wa kubuniwa kwa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania *(MKUKUTA).* Mkakati huo utatekelezwa kwa miaka mitano kuanzia mwaka 2005/2006 na unalenga katika kutoa kipaumbele kwenye suala zima la kukuza uchumi kama nyenzo muhimu katika kupunguza umaskini na kuleta maendeleo ya kijamii. *MKUKUTA* utaimarisha utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo mwaka 2025, kwa kuboresha mawasiliano na ushirikiano kati ya Sekta mbalimbali katika ukuzaji wa uchumi na maendeleo ya kijamii.

Mheshimiwa Spika, kutokana na Mkakati huo mpya, mgao wa fedha unaelekezwa katika Sekta zote kwa kutambua kwamba kila Sekta ni sehemu muhimu katika kukuza uchumi na kuondoa umaskini nchini. *MKUKUTA* unabainisha maeneo makuu matatu yanayolenga katika matokeo yanayotokana na mchango wa ushirikishwaji na maingiliano katika utendaji wa Sekta mbalimbali. Maeneo hayo ni:-

(i) Ukuaji Uchumi na Kupunguza Umaskini wa Kipato;

(ii) Uimarishaji wa Hali ya Maisha na Maendeleo ya Jamii;

(iii) Utawala bora na Uwajibikaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetayarisha mkakati huu kwa kutumia uzoefu uliotumiwa na nchi za Kusini Mashariki ya Asia ili kuweza kuharakisha zaidi ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini nchini na hivyo kuyafikia mapema zaidi malengo ya Dira ya Taifa mwaka 2025. Mkakati huu una sehemu kuu nne za utekelezaji zifuatazo:-

(i) Kujenga mazingira mazuri zaidi ya kuvutia kwa wingi uwekezaji kutoka nje na ndani ya Tanzania kwa kuanzisha maeneo maalum ya uwekezaji (*Special Economic Zones – SEZs*). Kwa lengo hili Serikali yenyewe itajenga miundombinu ya msingi katika maeneo hayo ili kupunguza gharama za kuanzisha miradi ya sekta binafsi na hivyo kuvutia uwekezaji zaidi;

(ii) Kuweka mfumo wa usimamizi na uendeshaji wenye uwezo wa kusimamia utekelezaji kwa ufanisi zaidi na kutatua haraka matatizo yatakayojitokeza;

(iii) Kuboresha mazingira ya kisheria; na

(iv) Kutangaza kwa nguvu fursa za *Special Economic Zones* na fursa nyingine ili kuwavutia wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa kulinganisha na nchi za Kusini Mashariki mwa Asia, Tanzania inazo sifa za kuiwezesha kufanikiwa. Kwa kuwa Tanzania inayo misingi mizuri ya sera za uchumi, uanzishaji wa *Special Economic Zones* zenye huduma zote muhimu na zinazoendeshwa kwa sheria zenye mvuto wa kutosha kwa wawekezaji utaleta matokeo mazuri kiuchumi. Kwa tathmini za awali, imeonekana ni vizuri kuanza na *Special Economic Zones* za Viwanda vya Nguo *(garment & textile)* na viwanda vingine vyenye ajira kubwa, *Special Economic Zones* za utalii na kilimo, *Special Economic Zones* za kupanda miti kwa ajili ya *pulp*, karatasi na *wood chips* na *Special Economic Zones* za kukata na kusafisha madini kuyaongezea thamani.

Mheshimiwa Spika, mkakati huu unakusudia kuiwezesha Tanzania kufikia haraka zaidi malengo ya ukuaji wa uchumi, mchango wa sekta ya viwanda kwenye pato la Taifa, mapato ya fedha za kigeni yatokanayo na bidhaa zinazouzwa nje, pato la wastani la Mtanzania na ajira mpya.

Mheshimiwa Spika, katika azma ya kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji, mashauriano yaliendelea kwa njia ya Mikutano kati ya Serikali, sekta binafsi, Mabalozi, wanataaluma na Mashirika ya Kimataifa chini ya Baraza la Taifa la Biashara. Mwaka 2003, Baraza lilifanya Mikutano ya Wawekezaji kwa kushirikiana na Kamati zilizoundwa za masuala ya kilimo, viwanda na usindikaji wa mazao ya kilimo, utalii na kuitangaza nchi, uendelezaji wa wataalam, fedha na biashara, pamoja na Kamati ya Ushauri kwa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliendelea kutekeleza Programu ya Kuimarisha Mazingira ya Biashara Tanzania *(Business Environment Strengthening for Tanzania Programme - BEST)*. Chini ya programu hiyo yafuatayo yamefanyika:-

1. Sheria ya Ardhi *(Land (Amendment) Act 2004)* ilifanyiwa marekebisho na kuifanya ardhi kuwa dhamana ya kuchukulia mikopo kwenye vyombo vya fedha;

2. Marekebisho ya Awamu ya Kwanza ya Sheria za Kazi *(Phase I Review of Labour Law Reforms)* yalifanywa ambayo yalipelekea kutungwa kwa Sheria ya Ajira ya mwaka 2004 *(Employment and Labour Relations Act 2004)* na Sheria ya Taasisi za Kazi *(Labour Institutions Act 2004);* na
3. Maandalizi ya kuboresha mfumo wa leseni na kodi za biashara pamoja na uwekezaji yameanza kwa lengo la kuongeza mapato.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha zaidi mazingira ya uwezeshaji wa wananchi kwa kutumia rasilimali zilizopo, Serikali imeandaa mkakati wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara ili wananchi waweze kuzitumia kama dhamana ya kukopa kutoka Taasisi za fedha kwa ajili ya kukuza shughuli zao za kiuchumi na hatimaye kupunguza umaskini. Katika kutekeleza mkakati huu unaojulikana kwa ufupi *MKURABITA,* kazi ya kurasimisha rasilimali imeshaanza hususan katika Mkoa wa Dar es Salaam na Mbeya. Aidha, Serikali imeunda Kamati ya Uendeshaji chini ya Mheshimiwa Anne Makinda, Mbunge, kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa mkakati huu kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, misingi na matarajio ya Mpango wa Muda wa Kati na Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha 2005/2006 - 2007/2008 ni pamoja na matumaini ya hali ya hewa nzuri, itakayoleta mafanikio katika kilimo na hivyo kuwa na uhakika wa chakula; kuendelea kuwa na amani na utulivu nchini; kuwa na fikra za maendeleo, tabia ya kujituma, nidhamu na kukubali mabadiliko vitaendelea kujitokeza na kukomaa miongoni mwa jamii zetu na kuwa chachu ya maendeleo na kupata rasilimali za kutosha kwa ajili ya kutekeleza malengo ya mpango.

Mheshimiwa Spika, malengo ya uchumi jumla katika kipindi cha mwaka 2005/2006 - 2007/2008 yatakuwa kama ifuatavyo:-

1. Pato halisi la Taifa kukua kwa asilimia 6.9 mwaka 2005, asilimia 7.2 mwaka 2006, asilimia 7.6 mwaka 2007 na asilimia 7.9 mwaka 2008;

2. Kiwango cha kasi ya upandaji bei kisichozidi asilimia 4.0 (kwa bei za 2001) kufikiwa ifikapo mwezi Juni 2006;

3. Mapato ya ndani kuongezeka kufikia asilimia 14.3 ya pato la Taifa mwaka 2005/2006, asilimia 14.5 mwaka 2006/2007 kuongezeka hadi asilimia 14.6 mwaka 2007/2008; na

4. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana *(M2)* kudhibitiwa kwa viwango vinavyowiana na malengo ya ukuaji wa uchumi na kasi ya upandaji bei; na
5. Akiba ya fedha za kigeni itakayokidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi saba.

Mheshimiwa Spika, tafsiri za shabaha kuu za kutekeleza malengo mapana ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2005/2006 ni:-

1. Kutengemaza uchumi mkuu;

2. Kutekeleza *MKUKUTA* ikiwa ni pamoja na kuendelea kutekeleza miradi mikubwa kama *MKURABITA*, Mkakati Maalum wa Kuharakisha Maendeleo Tanzania, Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Shinyanga-Kahama, Ujenzi wa barabara na madaraja pamoja na miundombinu ya umwagiliaji maji;

3. Kuimarisha na kusaidia sekta isiyo rasmi ili ipanuke na kutengemaa kwa lengo la kuingizwa kwenye mfumo rasmi wa uchumi;

4. Kufanikisha Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2005;

5. Kuimarisha mifumo ya uratibu na usimamizi wa miradi ya maendeleo katika ngazi zote; na

6. Kuendelea kutekeleza sera ya Serikali ya kupeleka madaraka kwa wananchi kupitia Programu ya Maboresho ya Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo ya hali ya uchumi wa Taifa pamoja na misingi, matarajio na malengo ya bajeti, napenda kuchukua fursa hii kusisitiza mambo muhimu ambayo kama Taifa tunahitaji kuyapa kipaumbele katika utekelezaji na ufuatiliaji.

Kwanza ni kuhakikisha kwamba wananchi wanaelewa masuala muhimu yote yaliyobainishwa katika *MKUKUTA*;

Pili, kutekeleza mipango, mikakati na malengo tuliyojiwekea yanayolenga katika kukuza uchumi na kuongeza tija, mapato ya fedha za kigeni, mapato ya ndani na ajira;

Tatu, kupeleka baadhi ya madaraka ya Serikali Kuu kwa Serikali za Mitaa kwa lengo la kuwapa wananchi uwezo wa kupanga na kutekeleza mipango na mikakati inayolenga katika kuwaondolea umaskini;

Nne, kuhakikisha kwamba sekta isiyo rasmi inarasimishwa kwa lengo la kuingizwa kwenye mfumo rasmi wa uchumi;

Tano, kuimarisha ufuatiliaji na tathimini ya utekelezaji wa mipango na mikakati ya maendeleo;

Sita, kukuza masoko ya ndani na nje kwa mazao ya biashara kwa kuzingatia ubora, viwango na ufungaji na kubuni mbinu za kuongeza uzalishaji wa mazao ya biashara pamoja na kutumia fursa zitokanazo na ushirikiano wa kikanda na Kimataifa;

Saba, kuendelea kuhimiza wawekezaji wa ndani na wa nje kuwekeza katika viwanda vidogo na vya kati vya kusindika mazao ya kilimo ili kuongeza thamani ya mauzo nje na kuchangia katika kupanua nafasi za ajira; na

Nane, kuendeleza mikakati ya kitaifa ya kujitosheleza kwa chakula.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha awamu ya tatu tumeweza kupata mafanikio mengi katika kukuza uchumi wetu. Hata hivyo, ili kuweza kufikia malengo ya Dira ya Taifa 2025 na kuweza kulingana na nchi zenye kipato cha kati, uchumi wa nchi unatakiwa kukua kwa kiwango kisichopungua asilimia nane juu ya kiwango cha ongezeko la idadi ya watu. Kiwango cha ongezeko la idadi ya watu kinakua kwa asilimia 2.9. Hivyo, hatuna budi kuboresha na kuendelea kusimamia utekelezaji wa sera na mikakati yetu ili tuweze kufikia malengo makuu ya Dira ya Taifa mwaka 2025 kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuelezea kuwa tegemeo kubwa la kuleta mabadiliko ya kiuchumi nchini liko kwa wananchi wenyewe ambao wanatakiwa kutumia fursa zilizopo na kukabili vikwazo kwa lengo la kuongeza tija kwa kasi kubwa na kukuza uchumi wetu ili tuondokane na umasikini tulionao. Hivyo, ni wajibu wa kila mmoja wetu kuchukia umasikini na kuhimizana kufanya kazi kwa bidii na kutumia kwa umakini, fursa na rasilimali zilizo katika uwezo wetu ili kujiletea maendeleo. Serikali itaendelea na jukumu la kuunga mkono juhudi za wananchi kwa kuandaa sera na mikakati ya kuelekeza namna ya kuratibu, kusimamia pamoja na kutathmini ili tuwe na maendeleo yenye kuwiana katika kila ngazi. Nina hakika kuwa kila mmoja wetu akitimiza wajibu wake sawasawa tutakuwa na kasi ya ukuaji wa uchumi unaopanda mwaka hadi mwaka na kufikia malengo yetu ya Dira ya Taifa mwaka 2025 na kufanikisha kupunguza umasikini kwa kiwango kikubwa. Hakika, Serikali ya Awamu ya Nne itayalinda na itayaendeleza mafanikio ya Awamu ya Tatu kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sera na msimamo wa Serikali ni kudumisha ushirikiano mzuri wa kidiplomasia uliopo kati yetu na nchi karibu zote duniani pamoja na taasisi za Kimataifa na Mashirika mbalimbali kwa manufaa yetu sote.

Kwa hiyo, tutakuwa tumekosa fadhila tusipotambua misaada na michango ya baadhi ya nchi, taasisi za kimataifa na Mashirika mbalimbali walioshirikiana nasi katika harakati za kuinua uchumi wetu na katika mapambano ya kuondoa umaskini. Naomba sasa nichukue fursa hii kuwashukuru wote waliotusaidia na kutoa pongezi zetu za dhati kwa kuzitaja nchi, Taasisi na Mashirika kama ifuatavyo:-

Serikali za Uswiss, Uholanzi, Ujerumani, Ufaransa, Uingereza, Hispania, China, Afrika ya Kusini, Japan, Kuwait, Italia, Ireland na nchi nyingine marafiki. Benki ya Dunia, Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF)*, Mashirika mbalimbali ya Umoja wa Mataifa kama vile *UNDP, UNESCO, UNFPA, UNHCR, UNICEF, UNIFEM, FAO, IFAD, WFP* na *WHO*, Jumuiya ya Nchi za Ulaya *(EU)*, Mfuko wa Fedha wa Nchi Wanachama wa Uzalishaji Mafuta *(OPEC Fund)*. Shirika la Maendeleo la Norway *(NORAD)*, Shirika la Maendeleo la Marekani *(USAID),* Shirika la Maendeleo la Sweden *(SIDA)*, Shirika la Maendeleo la Finland *(FINNIDA),* Shirika la Maendeleo la Denmark *(DANIDA),* Shirika la Maendeleo la Japan *(JICA),* Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)* na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa yasiyo ya Kiserikali *(NGOs)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kasi mpya, nguvu mpya na ari mpya.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge Kikao cha asubuhi kinaishia hapo. Tutakaporejea kipindi cha jioni tutaanza saa 10.00 ndivyo kanuni zetu zinavyosema kwamba siku ya Bajeti Kikao kinarudia saa 10.00 badala ya saa 11.00 ile ya kawaida.

Sasa tutakapokuja saa 10.00 kusikiliza hotuba ya Bajeti kuna wageni ambao tumewaalika na ni tabia yetu ya kila mwaka siku ya Bajeti ni siku muhimu katika Taifa lolote lile. Kwa hiyo, huwa tunawaalika makundi yafuatayo ya wageni wawepo kwenye *gallery*.

Kundi la kwanza ni Wageni wa Mheshimiwa Rais wetu Benjamini William Mkapa, ana wageni watatu wafuatao:- Mgeni wake wa kwanza ni Mheshimiwa Michel Camdessus anakuja pamoja na mkewe. Mheshimiwa Rais aliniomba waruhusiwe kuingia kwenye *gallery* ili wasikilize Bajeti, ni Mheshimiwa huyo na Mkewe. Wa tatu, ni Mheshimiwa Dr. Essop Pahad ni Waziri wa Nchi, katika Ofisi ya Rais wa Afrika Kusini naye ni Mgeni wake anakuja watakuwepo leo. Lakini hasa kazi kubwa inayowaleta ni ile ya kesho mchana ya uzinduzi wa Ripoti ya Tume ya Afrika. Hilo kundi moja la wageni mashuhuri watatengewa viti maalum kwenye *gallery*.

Halafu baada ya kundi hilo kuna kundi la Mabalozi wanaowakilisha nchi zao hapa Tanzania. Hatujapewa na Mkuu wa Mabalozi idadi kamili ya watakaokuja, lakini huwa tunawaalika wote sasa wenye nafasi wanakuja wasiokuwa na nafasi wanatuambia hivyo.

Kundi la tatu, ni Viongozi wa Serikali ngazi ya Mkoa wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa na wengineo. Kundi la nne, ni viongozi wa Vyama vya Siasa ambao huwa nao tunawaalika. Tunaalika Vyama vyote, wanaoweza kuja wanakuja wasioweza wanatuambia hivyo. Kundi lingine ni viongozi wa dini katika madhehebu ya *KKKT*, Anglikana, *BAKWATA* na Katoliki.

Kundi la mwisho huwa ni wazee wa Mji wa Dodoma kama 12 hivi wakiongozwa na Balozi Lusinde na wazee wenzake wengine.

Kwa hiyo, tutakuwa na wageni hao kwenye *gallery* ya leo kusikiliza hotuba ya Bajeti. Basi baada ya maelezo hayo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 10.00 Jioni.

*(Saa 05.19 Asubuhi Bunge lilifungwa mpaka saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** *Honourable Members before we start the session I would like to recognise the presence in the gallery of some very distinguished and special guests who are guests of President Benjamin Mkapa and they are sitting in the gallery this afternoon to listen to the budget speech.*

*I want to recognise the presence of the Former Managing Director of the International Monetary Fund, Mr. Michel Camdessus and Mrs. Camdessus. (Applause)*

*I also wish to recognise the presence in the gallery of Honourable Dr. Essop Pahad who is Minister of State in the Office of the President of South Africa. (Applause)*

*Also sitting in the same gallery are eleven Ambassadors and High Commissioners who are representing their countries here in the United Republic of Tanzania. (Applause)*

## HOJA ZA SERIKALI

## MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI KWA MWAKA 2005/2006

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2005/2006. Pamoja na hotuba hii, kuna vitabu vinne vinavyoelezea kwa undani Bajeti yenyewe. Kitabu cha kwanza kinaelezea Makadirio ya Mapato, cha pili kinahusu Makisio ya Matumizi ya Kawaida kwa Wizara na Idara, kitabu cha tatu kinahusu Matumizi ya Halmashauri za Miji na Wilaya, kitabu cha nne ni cha Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo kwa Wizara, Idara, Mikoa na Halmashauri. Kadhalika, upo Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine kufanikisha matayarisho ya Bajeti hii. Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge lako Tukufu, pamoja na Kamati nyingine za Kisekta, zilifanya kazi nzuri sana kuchambua makisio haya kwa kina na kutoa ushauri ambao umezingatiwa katika Bajeti hii.

Aidha, napenda kuishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kutayarisha Miswada na nyaraka mbalimbali za Sheria ambazo ni sehemu ya Bajeti hii.

Napenda pia kuwashukuru wafanyakazi wenzangu wote wa Wizara ya Fedha, hususan Manaibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Alhaj Abdisalaam Issa Khatibu na Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, Makatibu Wakuu, Bwana Gray S. Mgonja na Bwana Peniel M. Lyimo, Naibu Katibu Mkuu, Bwana Ramadhani M. Khijjah, Wakuu wa Idara na wafanyakazi wote kwa kufanikisha maandalizi ya Bajeti hii.

Pia, namshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ambaye ameweza kuchapisha kwa wakati hotuba hii, vitabu vya Bajeti na nyaraka nyingine kwa ufanisi mkubwa. Nawashukuru wale wote waliowasilisha kwangu mapendekezo mbalimbali kuhusu kodi na kuhusu Sera za Mapato na Matumizi kwa ujumla. Ushauri wao umechangia sana tena kwa kiwango kikubwa katika kukamilisha Bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika miezi kumi na moja iliyopita, tumepoteza Wabunge wenzetu watano ambao waliaga dunia. Wabunge hao ni Hayati Mheshimiwa Yete Sintemule Mwalyego, aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini, Hayati Mheshimiwa Kepteni Theodos James Kasapira, aliyekuwa Mbunge wa Ulanga Mashariki, Hayati Mheshimiwa Frank Michael Mussati, aliyekuwa Mbunge wa Kasulu Mashariki, Hayati Mheshimiwa Balozi Ahmed Hassan Diria, aliyekuwa Mbunge wa Rahaleo na Hayati Mheshimiwa Abu Towegale Kiwanga, aliyekuwa Mbunge wa Kilombero. Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu hawa mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, hiki ni kikao cha mwisho cha Bajeti kwa Bunge hili la Awamu ya Tatu. Bajeti ya leo ni ya kumi tangu Serikali ya Awamu ya Tatu iingie madarakani mwezi Novemba, 1995. Wengi wetu tunarudi kwa wananchi kwa mujibu wa sheria na taratibu, kuomba ridhaa yao ya kurudi tena katika ukumbi huu ambao utakuwa mpya na mkubwa zaidi. Nina matumaini makubwa sana kuwa wananchi hawatasahau mema na makubwa mengi yaliyofanywa na Bunge la Awamu ya Tatu na Serikali yake.

Awamu ya Tatu chini ya uongozi wa Rais Benjamin William Mkapa imepata mafanikio makubwa na ya kujivunia hasa katika kufufua na kukuza uchumi, kuimarisha miundombinu na kutoa huduma kadhaa za jamii. Uwezo wa Serikali wa kutoa huduma za msingi za uchumi na za jamii umeongezeka zaidi ya mara tatu katika kipindi cha miaka tisa ya utawala wa Awamu ya Tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kulipongeza Bunge lako Tukufu chini ya uongozi wako, kwa mchango mkubwa ambao umeiwezesha Serikali ya CCM ya Awamu ya Tatu kufikia mafanikio makubwa. Aidha, nachukua fursa hii kumpongeza mwenzetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Mbunge wa CCM, Chalinze na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa kuteuliwa na CCM, kwa kura nyingi, kugombea nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa tiketi ya CCM. Chaguo hilo la CCM ni alama ya imani ya chama hicho kwetu sisi Wabunge na Bunge lenyewe kama taasisi na ni mfano unaostahili kuigwa na vyama vyote vya siasa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali, Bajeti hii ni ya kumi tangu Serikali ya Awamu ya Tatu iingie madarakani mwezi Novemba, 1995. Katika kipindi hicho, Bajeti ya Serikali imekuwa chombo muhimu cha kusukuma maendeleo ya nchi. Kwa kuweka misingi imara ya usimamizi wa Bajeti, hali ya uchumi kwa ujumla imekuwa tulivu kwa sababu tumejifunza kutumia kile tulichokuwa nacho.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka tisa iliyopita, Tanzania imepata mafanikio makubwa, licha ya vikwazo vingi kama vile mafuriko ya mvua za *El-nino,* ukame, kupanda kwa bei ya mafuta ya petroli katika soko la nje, kushuka kwa bei ya mazao ya kilimo katika soko la dunia na mambo mengine mengi. Licha ya vikwazo hivi, Serikali ya Awamu ya Tatu imefanya mambo makubwa kwa lengo la kufanya maisha ya Watanzania yawe bora na salama. Baadhi ya mafanikio hayo ameyaeleza vizuri Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, leo asubuhi. Mengine yataelezwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wa kisekta watakapo wasilisha hoja zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa msisitizo, mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tatu ni pamoja na haya yafuatayo:-

(a) Kuweka misingi imara ya kukusanya mapato ya ndani na kwa kuwa na ushirikiano mzuri na wafadhili, na kusimamia Bajeti ya Serikali kwa ufasaha. Serikali imejenga uchumi tulivu.

(b) Kujenga nidhamu ya kutumia tulicho nacho bila kuchapisha noti ovyo. Tumeweza kushusha mfumuko wa bei kutoka asilimia 21 mwaka 1996 hadi kufikia asilimia 4 mwaka 2005.

(c) Kasi ya kukua kwa Pato la Taifa imeongezeka kutoka asilimia 4.2 mwaka 1996 hadi asilimia 6.7 mwaka 2004. Kasi hii ya kukua kwa uchumi inaiweka Tanzania kileleni miongoni mwa nchi nyingi za Afrika.

(d) Urari wa malipo ya nje umeimarika kwa kiwango kikubwa. Akiba ya fedha za kigeni sasa inatosha kununua bidhaa na huduma kutoka nje kwa mahitaji ya miezi 7 hadi 8, kulinganisha na miezi miwili miaka kumi iliyopita. Ingawa mauzo yetu katika Soko la Kimataifa hayajaongezeka kwa kiwango kikubwa, urari wa malipo ya nje umekuwa mzuri kwa sababu ya uwekezaji, misaada ya nje ambayo imeongezeka zaidi ya mara tatu, ikiwemo misamaha ya madeni, kukua kwa utalii na matokeo ya sera ya kuruhusu biashara huria ya fedha za kigeni.

(e) Kwa kuvutiwa na mazingira mazuri ya uwekezaji, sasa ziko benki za biashara 26 badala ya 2 tu zilizokuwepo mwaka 1996. Aidha, ziko taasisi nyingine tano za fedha kwa sasa badala ya mbili tu zilizokuwepo mwaka 1996. Mikopo ya benki imeongezeka na sasa inakua kwa kiwango cha asilimia 30 kwa mwaka. Riba ya mikopo imeshuka kwa wastani kutoka asilimia 26 mwaka 1996 hadi asilimia 14.4 mwaka 2004.

(f) Masoko ya fedha yamekua. Sasa liko soko la hisa, ziko kampuni za bima karibu kumi na vyombo vingine vingi ambavyo havikuwepo miaka kumi iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nguzo kuu ya uchumi endelevu ni akiba ya ndani ya nchi inayoambatana na uwekezaji. Akiba ya ndani inakusanywa kupitia njia mbili kuu, ambazo ni kodi na amana za wananchi na wafanyabiashara wanazowekeza katika vyombo vya fedha. Kodi ndio chanzo kikuu kinachoipa Serikali uwezo wa kuendeleza huduma za uchumi, huduma za jamii, ulinzi na usalama, pamoja na uwekezaji katika miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1995/1996 Serikali ilikusanya shilingi bilioni 448.4 kwa mwaka au shilingi bilion 37 kwa mwezi. Mwaka huu wa 2004/2005, Serikali inakusanya shilingi trilioni 1.774, sawa na shilingi bilioni 145 kwa mwezi. Hili ni ongezeko la zaidi ya mara nne katika kipindi cha miaka kumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ongezeko la ukusanyaji wa mapato limetokana na sera thabiti zilizotekelezwa katika kipindi hicho. Kwa muhtasari, mambo yafuatayo yalitekelezwa na Serikali ya Awamu ya Tatu kwa njia ya Kibajeti:-

(a) Sera za kodi na mfumo wake zilifanyiwa mageuzi makubwa, ambayo ni pamoja na kuwianisha na kuhuisha kodi mbalimbali kwa lengo la kurahisisha ukusanyaji wake.

(b) Idadi kubwa ya kodi zenye tija ndogo au zenye kero kwa wananchi zilifutwa ikiwemo kodi ya maendeleo.

(c) Kodi mpya ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* ilianzishwa mwaka 1997.

(d) Mianya ya kukwepa kodi, hasa ushuru wa forodha imezibwa kwa kiwango kikubwa.

(e) Usimamizi wa ukusanyaji mapato chini ya Mamlaka ya Mapato *(TRA)* umeimarishwa kwa kiwango kikubwa. Kwa mfano, sasa kuna Idara ya Walipa Kodi Wakubwa ambao wanasikilizwa kwa umakini mkubwa, jambo ambalo linaongeza ari ya wao kulipa kodi bila kusukumwa mno.

(f) Serikali imeanzisha utaratibu wa kujadiliana na walipa kodi kila mwaka kuhusu sera na viwango vya kodi. Utaratibu huu pia umesaidia kuongeza utiifu katika kulipa kodi kwa hiari.

(g) Sheria mbalimbali za kodi zimetungwa upya au zimerekebishwa, ili ziende na wakati.

(h) Utawala wa Mamlaka ya Mapato Tanzania umeimarishwa kwa kiwango kikubwa na bado unaendelea kuimarishwa.

(h) Bodi ya Rufaa za Kodi na Baraza la Rufaa za Kodi zilianzishwa mwaka 2000 kwa lengo la kusikiliza malalamiko ya walipa kodi.

(i) Taratibu za forodha zimeboreshwa na kuwa za kisasa. Kwa mfano mafuta ya petroli yanapoingizwa nchini kupitia Dar es Salaam yanapita kwenye kipimo maalum kinachojulikana kama *Flow Meter.*

Aidha, mizigo inayokuja kwenye makontena sasa inachujwa na mashine maalum inayoitwa *Container Scanner* ili kudhibiti ukwepaji kodi na mashine hii sasa imeingia kwenye kiwanja cha ndege cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi pamoja na nyingine, ndizo zinazoiwezesha Serikali kuongeza ukusanyaji wa mapato zaidi ya mara nne katika kipindi hicho. Ukusanyaji mzuri wa mapato ya ndani, pamoja na misaada na mikopo ya masharti nafuu kutoka kwa Nchi Marafiki na Mashirika ya Fedha ya Kimataifa, viliiwezesha Serikali kuwekeza kwa kiwango kikubwa katika programu za Afya, Elimu, Barabara, Maji, Kilimo na sekta nyinginezo. Katika kipindi hicho, mgao wa fedha za Bajeti kwa ajili ya sekta hizo uliongezeka karibu mara nne na matokeo ya hatua hizi yanaonekana katika sekta hizo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na sera sahihi za uchumi, utawala bora na uwajibikaji, ikiwepo nidhamu ya matumizi ya mali ya umma, tumerejesha uhusiano mzuri wa misingi ya ushirikiano *(partnership)* na wafadhili wetu na hivyo misaada ya nje imeongezeka zaidi ya mara tatu katika miaka kumi iliyopita. Misaada ya nje na mikopo

ya masharti nafuu imeongezeka kutoka shilingi bilioni 187 mwaka 1995/1996 hadi shilingi trilioni 1.7 mwaka huu.

Aidha, mkakati wa Serikali ya Tanzania wa kusimamia misaada umechangia katika ongezeko la misaada hasa ile inayopitia kwenye Bajeti yetu. Awamu hii ilipoingia madarakani, hakukuwa na misaada ya Bajeti. Misaada yote ilikuwa ikitolewa kwa njia ya miradi, ambayo kwa kiasi kikubwa ilikua inabuniwa na kusimamiwa na wafadhili wenyewe. Serikali haikuwa na uelewa wa mambo yanayotokea huko kwenye miradi. Utaratibu huo sasa umebadilika. Sisi wenyewe ndio tunabuni miradi na kusimamia utekelezaji wake. Sehemu kubwa ya misaada sasa inatolewa kupitia Bajeti ya Serikali kwa utaratibu unaoitwa *(Budget Support).* Hata Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika, zinatoa sehemu kubwa ya mikopo ya masharti nafuu kupitia Bajeti ya Serikali. Huu ni ushahidi tosha kwamba dunia ina imani na Serikali ya Mkapa kwani hili wanalifanya kwa nchi chache sana Afrika Kusini mwa Sahara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na sera sahihi za uchumi, imani ya Nchi Marafiki na Mashirika Wafadhili kwa Serikali ya Tanzania imetokana pia na mageuzi tuliyofanya katika usimamizi wa fedha na uwajibikaji wa Serikali. Uamuzi wa kuwekeza katika mfumo wa mtandao wa malipo Serikalini *(IFMS)* na mpango unaoendelea wa mageuzi ya usimamizi wa fedha za umma vimekuwa vichocheo muhimu vya sisi kuaminiwa na hao wanaotusaidia, kwa imani kwamba misaada yao itatumiwa kwa malengo tuliyokubaliana nao. Ushirikiano huu mzuri kati ya Tanzania na Wafadhili umekuwa unasimamiwa chini ya utaratibu ujulikanao kama Mkakati wa Tanzania wa Kusimamia Misaada *(Tanzania Assistance Strategy),* ambao sasa unaimarishwa zaidi na utakuwa unaitwa Mkakati wa Pamoja wa Kusimamia Misaada *(Joint Assistance Strategy - JAS).*

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tatu imeweka juhudi kubwa kushughulikia tatizo tulilokuwa nalo la mzigo wa madeni. Nchi yetu ilikuwa na limbikizo kubwa la deni ambalo halikuwa rahisi kulilipa kwa kuwa mapato yetu yalikuwa kidogo sana. Kwa maana hiyo, Tanzania ilikuwa haikopesheki tena. Ili kurejesha heshima ya Nchi, Serikali hii iliamua kujikokota kulipa baadhi ya madeni kidogo kidogo. Papo hapo Serikali iliungana na wadau wengine wa Kimataifa kutaka Nchi na Mashirika tajiri zifute madeni ya nchi maskini kama Tanzania. Serikali pia ilibuni sera na mkakati mpya wa Kitaifa wa kusimamia madeni. Katika kipindi hicho, walikuwepo baadhi ya watu waliohoji mantiki ya kulipa madeni wakati uchumi wetu ulikuwa dhaifu.

Mheshimiwa Spika, mkakati huo wa Serikali wa kulipa madeni ulizaa matunda pale Tanzania ilipoingizwa kwenye kundi la nchi maskini zenye madeni makubwa sana duniani *HIPC* ambazo zilistahili kufutiwa sehemu kubwa ya madeni ya nchi zao. Matokeo yake ni kwamba Tanzania imesamehewa madeni kiasi cha shilingi trilioni tatu yatakayoiva katika kipindi cha miaka ishirini ijayo. Hadi sasa tumeshafutiwa madeni yenye thamani ya takriban shilingi trilioni 1.3. Hadhi ya Tanzania Kimataifa imepanda na sasa nchi inakoposheka tena, kwa kuwa inao uwezo wa kulipa madeni yake. Sisi leo tunachagua wapi tukakope, kinyume na miaka ya nyuma ambapo tulikuwa hatukopesheki. Hata hivyo, tunatambua kwamba bado tuna madeni ya kulipa na kwa

kuwa nchi yetu ni changa, shinikizo la kutaka kufutiwa madeni yaliyobaki bado linaendelea.

Mheshimiwa Spika, jitihada za Serikali hazikuishia kwenye kusafisha taswira yake kwa nchi na taasisi za nje zinazotudai. Katika kipindi cha mwaka 1995/1996 hadi 2003/2004, madeni ya ndani yaliyofikia shilingi bilioni 144.3 yamehakikiwa na kulipwa. Kiasi hiki kinajumuisha fidia ya shilingi bilioni 12.3, madeni ya wazabuni shilingi bilioni 111 na limbikizo la mishahara ya watumishi wa Serikali, kama vile walimu shilingi bilioni 21. Hatua hii ilisaidia kuzindua sekta binafsi ya ndani ambayo ilikuwa imeathirika kutokana na kucheleweshewa malipo yao. Aidha, madeni mengine ya ndani yakiwemo ya fidia mbalimbali yanaendelea kuchambuliwa na kuhakikiwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho cha miaka 10 cha Serikali ya Awamu ya Tatu, hatua nyingi za kuwawezesha wananchi kumiliki uchumi wao na kujiletea maendeleo yao zimetekelezwa, kama ifuatavyo:-

(a) Serikali imetunga Sera ya Uwezeshaji wa Wananchi kiuchumi, na Bunge limetunga Sheria ya kutekeleza Sera hiyo, na hivi sasa imeanza kutekelezwa.

(b) Serikali ilibuni na kusimamia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* ambao unawashirikisha kwa karibu sana wananchi kupitia Serikali za Vijiji katika kubuni na kupanga miradi ya maendeleo. Mradi huu umekuwa na mafanikio makubwa sana. Hivi majuzi, Awamu ya Pili yenye Bajeti ya takriban shilingi bilioni180 imezinduliwa na Mheshimiwa Rais Kitaifa Wilayani Magu. *(Makofi)*

(c) Aidha, Serikali imebuni, inatafiti na inatekeleza programu maalum ya kurasimisha raslimali za sekta isiyo rasmi ili kuwawezesha wananchi kutumia raslimali zao kama dhamana ya kukopa kutoka benki.

(d) Kama nilivyosema awali, Serikali imebuni Sera ya Taifa ya Mikopo Midogo Midogo *(National Micro Finance Policy)* ya mwaka 2001. Taratibu na Kanuni za utekelezaji wa sera hiyo zimekamilika na kuchapishwa. Wananchi wengi wa kipato cha chini wanategemewa kufaidika na mpango huu.

(e) Serikali kwa kushirikiana na Benki Kuu imeanzisha Mfuko wa Udhamini wa Mikopo ya benki kwa ajili ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi *(Export Credit Guarantee Scheme-ECGS).* Mfuko huu unasaidia sana hasa vyama vya ushirika kununua mazao ya biashara kwa wakulima na kuuza nje ya nchi. Wawekezaji katika maeneo maalum ya kuzalisha na kuuza nje *(EPZ)* pia wanafaidika na Mfuko huu.

(f) Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeanzisha Mfuko wa kudhamini mikopo ya benki kwa wawekezaji wadogo na wa kati, ambapo kiasi cha Shilingi 2.0 bilioni zimekwishatolewa hadi sasa. Aidha, Serikali iko karibu kukamilisha uanzishwaji wa Mfuko wa Dhamana ya Mikopo ya muda mrefu.

(g) Serikali imetekeleza mageuzi makubwa katika sekta ya mabenki na taasisi za fedha nchini ambayo yatawanufaisha sana wateja.

(h) Pamoja na mageuzi hayo, zoezi la kuirekebisha Benki ya Rasilimali *(TIB)* ili iweze kuwa benki ya maendeleo sasa liko katika hatua za mwisho. Aidha, zoezi linaendelea pia la kuiwezesha mifuko ya hifadhi ya jamii kutoa mikopo ya muda mrefu na mikopo ya nyumba kupitia benki na vyombo vingine vya fedha.

(i) Wakati huo huo, Serikali inashirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Makazi *(HABITAT)* kutengeneza mazingira ya kuwezesha kupatikana mikopo ya nyumba.

(j) Serikali inashirikiana pia na Shirika tanzu la Benki ya Dunia *(IFC)* pamoja na baadhi ya Nchi Wafadhili kujenga mazingira ya kuwezesha ukopeshaji wa vifaa *(leasing)* hasa vifaa vya uzalishaji. Mpango huu, unaohusisha *IFC,* Serikali ya Switzerland na Serikali ya Tanzania, kwa kuanzia, ulizinduliwa mwezi Mei, 2005.

(k) Katika hatua za kuimarisha Benki Kuu ya Tanzania na kuiongezea uwezo wa kusimamia sekta ya benki, Serikali itawasilisha katika Bunge hili mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwaka 1995, na Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 1991.

(l) Taratibu za utekelezaji wa mabadiliko ya Sheria ya Ardhi ya mwaka 2004 zitasaidia mikopo mingi kutolewa na mabenki kwa kutambua umilikaji wa ardhi kama dhamana *(collateral)* halali kwa mabenki wakati wa utoaji mikopo.

(m) Kuanzishwa kwa Soko la Hisa la Dar es Salaam *(Dar es Salaam Stock Exchange - DSE)* pamoja na Mamlaka ya Soko la Mitaji *(Capital Markets & Security Authority - CMSA)* kunaweka mazingira mazuri ya ushiriki wa wananchi katika kumiliki hisa. Hivi sasa wananchi zaidi ya 67,000 wanamiliki hisa za kampuni mbalimbali zilizoorodheshwa katika soko hilo.

(n) Serikali inatekeleza Mpango wa Kupanua Huduma za Fedha Vijijini *(RFSP),* kwa kuweka kanuni za uendeshaji wa Benki Kata na vyombo vingine vidogo vya wanachama vya kuweka na kukopa *(member - based micro credit entities).* Kuanzia sasa vikundi hivyo vitasimamiwa kwa miongozo itakayotolewa na Benki Kuu ya Tanzania kitaifa kwa msingi wa sera za Serikali na za uendeshaji bora *(best practice)* wa taasisi za aina hii. Benki Kuu inategemewa kukasimu madaraka yake kwa Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri na Idara zao za Maendeleo ya Jamii, ambao watapewa madaraka ya kuandikisha vikundi hivyo kisheria hapo hapo Wilayani na kuvitekelezea wajibu wa kitaalamu na kiutawala kama itakayoelekezwa.

Hatua hii itaondoa utata uliojitokeza kwa baadhi ya watendaji kutoelewa hali ya vikundi kuwa vya ushirika *(SACCOs)* chini ya sheria ya ushirika na visivyo ushirika *(SACAs)* ambavyo kuanzia sasa taratibu hizi ambazo pia ni za kisheria zitatumika kuviandikisha na kuvihudumia chini ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya kwa kutumia Idara zake za Ushirika kwa *SACCOs* na Maendeleo ya Jamii kwa *SACAs* au Benkikata.

Ni vema ifahamike kuwa ndani ya Wilaya moja *SACCOs* na *SACAs*/Benkikata zinaweza kuungana kuunda Benkikata kubwa au Benki ya Wananchi iliyo kubwa zaidi. *(Makofi)*

(o) Mfuko wa Dhamana ya Uwekezaji *(Unit Trust of Tanzania) - UTT)* ambao ulianzishwa mwaka 2003 chini ya Sheria ya Udhamini, umeanza kufanya kazi kikamilifu. Baada ya maandalizi kukamilika, utaratibu wa uwekezaji chini ya *UTT* kwa jina la Mfuko wa Umoja *(Umoja Fund)* umeanza tarehe 16 Mei, 2005 ambapo wananchi sasa wana fursa ya kuwekeza kwenye mfuko huo kwa kununua dhamana *(units)* au vipande tunasikia kwenye redio. Ili kufanikisha malengo ya Mfuko, Serikali imefanya yafuatayo kwa dhamira ya uwezeshaji:-

(i) Imetoa asilimia 2 ya hisa zake katika Kampuni ya Bia Tanzania *(TBL)* na asilimia 1 katika Kampuni ya Sigara Tanzania *(TCC)* kama mtaji wa mwanzo wa Mfuko wa Umoja. Hisa hizo zina thamani ya shilingi bilioni 10.9.

(ii) Imetoa punguzo la asilimia 30 katika bei ya dhamana *(units)* za mfuko ili kuwezesha wananchi wengi kumiliki dhamana za Mfuko wa Umoja.

(iii) Dhamana zinauzwa kwa raia wa Tanzania, kampuni zinazomilikiwa na raia na Mifuko ya Akiba ya Uzeeni ya hapa nchini tu. Benki hazitaruhusiwa kushiriki katika hatua ya mwanzo ya Mfuko. Mheshimiwa Spika, hatua za kuondoa kero kwa Wananchi, pamoja na hatua hizo nilizoeleza, Serikali pia imetekeleza hatua za makusudi za kupunguza tofauti za mapato katika jamii na kuondoa kero mbalimbali zinazowakabili wananchi. Hatua hizo ni pamoja na hizi zifuatazo:-

(i) Ada zote katika shule za msingi zimefutwa ili kuwawezesha watoto wote wenye umri wa kwenda shule kuandikishwa. Hii ilikuwa hatua kubwa na ya kimapinduzi. Aidha, ada katika Shule za Sekondari za Kutwa za Serikali zimepunguzwa kutoka shilingi 40,000/= hadi shilingi 20,000/= kwa mwaka. Hili nalo ni la kimapinduzi. *(Makofi)*

(ii) Kodi na ada mbalimbali zinazowaletea kero wananchi, ikiwemo kodi ya maendeleo, zimefutwa. Hili lilikuwa la Kimapinduzi zaidi. *(Makofi/Kicheko)*

(iii) Serikali inatoa ruzuku ya usafirishaji wa mbolea kwa manufaa ya wakulima. Hili ni la mapinduzi vijijini. *(Makofi/Kicheko)*

(iv) Kodi za zana za kilimo zinazoagizwa kutoka nje ya nchi kama matrekta zimefutwa ili kupunguza gharama za uzalishaji. *(Makofi)*

(v) Serikali inatoa bure huduma ya tiba katika hospitali na vituo vya afya kwa wanawake wajawazito na watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano na wagonjwa wa Ukoma, Kifua Kikuu na Ukimwi. *(Makofi)*

(vi) Mishahara ya Watumishi wa Serikali imeongezwa ambapo kima cha chini cha mishahara ya Watumishi wa Serikali kimeongezwa kutoka shilingi 17,500/= kwa mwezi mwaka 1995 hadi Shilingi 60,000/= kwa mwezi mwaka 2004; na

(vii) Wastaafu waliolipwa pensheni kwa mtindo wa mkupuo wamerejeshwa katika daftari la pensheni ili kuwasaidia kumudu hali ya maisha. Kima cha chini cha pensheni pia kiliongezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio mengi ya kiuchumi na fedha ya Serikali ya Awamu ya Tatu, nchi yetu bado inakabiliwa na changamoto nyingi, zikiwemo zifuatazo:-

(i) Nchi yetu bado ni maskini sana. Tukizingatia kwamba idadi ya watu inaongezeka kwa karibu asilimia 3 kwa mwaka, tunalazimika kuongeza kasi ya kukua kwa uchumi hadi asilimia 10 kwa mwaka ili tufikie lengo la dira ya Taifa ya kufikia kiwango cha mapato za kuitwa nchi zenye uchumi wa kati *(Middle Income Country)* mwaka 2025. Ubunifu zaidi, ari mpya na kasi mpya ya kweli vinahitajika ili kuongeza kasi ya kukua kwa uchumi. Hii ni changamoto kubwa inayolikabili Taifa kwa sasa. *(Makofi)*

(ii) Bajeti ya Serikali bado ni tegemezi kwa asilimia 41 lakini utegemezi huu umekuwa ukishuka mwaka hadi mwaka. Kwa hiyo, tunalo jukumu kubwa la kuongeza zaidi ukusanyaji wa mapato ya ndani. Pamoja na kuimarisha Mamlaka ya Mapato na kuboresha ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi, kasi kubwa zaidi ya kukua kwa uchumi ndio mkakati mkuu utakaofanikisha azma yetu ya kujitegemea. *(Makofi)*

(iii) Sehemu kubwa ya mapato yetu ya fedha za kigeni inatokana na misaada na mikopo ya masharti nafuu kutoka nje. Mauzo ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi ni kidogo sana. Ni lazima tuweke nguvu mpya katika kukuza mauzo ya nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tatu, napenda sasa kurejea katika utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2004/2005. Kama alivyoeleza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, uchumi umekua kwa asilimia 6.7 mwaka huu wa fedha 2004, mfumuko wa bei umeshuka kutoka asilimia 4.8 mwezi Machi, 2004 hadi kufikia asilimia 4.1 mwezi Machi, mwaka huu 2005 na unatarajiwa kukufikia lengo la asilimia 4.0 mwisho wa Juni 2005. Akiba ya fedha za kigeni, hadi Machi 2005, ilikuwa inatosheleza kulipia mahitaji ya bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi cha miezi 8.3, ikilinganishwa na lengo la miezi 6 ifikapo Juni mwaka huu 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2004/2005, Serikali ilidhamiria kupanua wigo wa kodi na kuimarisha usimamizi na utawala wa Mamlaka ya Mapato, hasa kupanua Idara ya walipakodi wakubwa; kutekeleza Sheria mpya ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004, kufanya mapitio ya sheria mbalimbali za kodi, ikiwemo Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT),* kwa lengo la kuziboresha. Aidha, Serikali ilitangaza hatua kadhaa za motisha ya kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya kilimo na

kurahisisha biashara kwa kurekebisha mfumo wa leseni za biashara na kutekeleza Itifaki ya Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa Bajeti ya 2004/2005 hadi Machi 2005 unaonyesha matokeo ya kuridhisha. Ukusanyaji wa mapato umevuka lengo na matumizi yameendelea kuwa chini ya lengo, japo kwa kiasi kidogo zaidi ya miaka ya nyuma. Aidha, mikopo na misaada ya Bajeti imepatikana kwa wakati kama ilivyotegemewa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004/2005, Serikali ilipanga kukusanya mapato ya ndani ya jumla ya shilingi 1,739,288 milioni sawa na asilimia 13.8 ya Pato la Taifa. Katika kipindi cha Julai, 2004 hadi Machi 2005 mapato yalifikia shilingi 1,314,524 milioni ambayo ni shilingi 21,681 milioni au asilimia 2 zaidi ya makadirio ya shilingi 1,285,257 milioni kwa kipindi hicho. Mwelekeo unaonyesha kuwa lengo la mapato kwa mwaka 2004/2005 litafikiwa na kuvukwa kidogo. Matokeo ya hatua mbalimbali za kodi zilizochukuliwa mwaka 2004/2005 pia ni ya kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, sehemu kubwa ya ongezeko la mapato imechangiwa na kodi ya ongezeko la thamani *(VAT)* na kodi ya mapato. Ukusanyaji wa *VAT* uliongezeka kutokana na hatua ya kupandisha thamani ya Kampuni zinazotakiwa kujisajili kwa *VAT* kutoka shilingi milioni 20 kwa mwaka hadi shilingi milioni 40. Kwa maana nyingine, idadi ya walipa kodi ya *VAT* imepungua na hivyo kuongeza ufanisi katika ukusanyaji. Ongezeko la ukusanyaji wa kodi ya mapato limetokana na kodi ya ajira *(PAYE)* na kodi ya makampuni *(Corporation Tax),* kutokana na ufanisi wa ukusanyaji na kuziba mianya ya ukwepaji kodi, hasa katika kodi ya mapato, kwa sababu ya sheria mpya ya 2004.

Sababu nyingine ni pamoja na kuanzisha kituo kimoja cha kulipia kodi za aina zote *(one stop centre)* katika kila Wilaya, na pia kwa kupanua Idara ya Walipa Kodi Wakubwa ambayo imeboresha huduma kwa walipa kodi. Aidha, matumizi ya teknolojia ya kisasa pamoja na mafunzo kwa watoza kodi vimerahisisha ukusanyaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Ushuru wa Forodha, makusanyo halisi hayakufikia lengo kutokana na sababu mbalimbali. Aidha, ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi *(Non-tax-revenue)* ikijumuisha mapato yanayokusanywa na Wizara, Idara na Mikoa yalivuka lengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi nyingi wahisani na mashirika ya fedha ya Kimataifa yameitikia wito wa kutupatia misaada kuchangia harakati zetu za kukuza uchumi na kuondoa umaskini. Katika kipindi cha Julai, 2004 hadi Machi, 2005, misaada na mikopo kwa ajili ya bajeti ilifikia shilingi 429,676 milioni ikiwa ni shilingi 4,800 milioni au asilimia 1.1 tu chini ya makisio ya shilingi 434,476 milioni katika kipindi hicho. Hali kadhalika, jumla ya shilingi 719,817 milioni zilipatikana katika kipindi hicho kama misaada na mikopo ya masharti nafuu kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kiasi hiki ni shilingi 134,442 milioni au asilimia 23 zaidi ya makisio ya shilingi 585,376 milioni katika kipindi hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2004 hadi Machi 2005, Serikali ilipanga kupunguza akiba yake kutoka Benki Kuu kwa shilingi 118,200 milioni ili kugharamia matumizi yaliyopangwa. Hata hivyo, kutokana na ukusanyaji mzuri wa mapato ya ndani, Serikali haikupunguza akiba yake na badala yake akiba iliongezeka kwa shilingi 81,368 milioni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hadi Machi 2005, matumizi yalifikia jumla ya shilingi 2,429,269 milioni ikilinganishwa na makisio ya shilingi 2,486,892 milioni katika kipindi hicho. Shilingi 1,560,067 milioni ni matumizi ya kawaida na shilingi 869,202 milioni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Katika matumizi ya kawaida, shilingi 152,122 milioni zimetumika kulipia madeni. Mishahara kwa watumishi wa Serikali ilikuwa shilingi 409,333 milioni ikilinganishwa na makisio ya shilingi 413,369 milioni. Kadhalika, madai halali ya walimu na watumishi wengine wa Serikali yaliyohakikiwa yamelipwa kama ilivyopangwa. Ili kudhibiti malimbikizo ya madai kama haya, utaratibu wa kuzuia malimbikizo ya mishahara ya watumishi wa Serikali, wakiwemo walimu, unaimarishwa, kama ulivyofafanuliwa katika Waraka wa Hazina Na. 12 wa Mwaka 2004 uliosambazwa kwa Maafisa Wahasibu wote nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha usimamizi na uwajibikaji katika matumizi ya fedha na mali za umma. Serikali imetunga Sheria mpya ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2004 ili kupanua madaraka na uwajibikaji ndani ya sekta ya umma. Utaratibu wa kutumia tulichonacho *(Cash Budget)* umeendelea kutumika katika kusimamia na kudhibiti matumizi ya Serikali.

Mtandao wa kompyuta wa kusimamia malipo *(IFMS)* umeendelea kuimarishwa kwa kufunga vifaa vya tahadhari pindi mtandao uliopo ukipata matatizo *(disaster recovery site)*. Mtandao huo unahakikisha kwamba, matumizi yanazingatia Bajeti iliyopitishwa na Bunge na kwamba, ubadhirifu unabainishwa kwa haraka na kwa uhakika zaidi kuliko ilivyokuwa kabla ya mtandao huo. Baada ya kuunganisha Maafisa Wahasibu wote wa Wizara na Idara zinazojitegemea, hivi sasa mtandao umefikishwa katika Ofisi za Katibu Tawala wa Mikoa yote Tanzania Bara na pia katika Halmashauri 32 za Wilaya. Aidha, mafunzo kwa Wahasibu wa Serikali yanaendelea. Vile vile, Serikali imewarejesha wastaafu 10,813 waliokuwa wamechukua mafao yao kwa mkupuo katika Daftari la Pensheni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mwenendo wa Bajeti wa mwaka wa fedha hadi mwezi Machi 2005, Serikali inaamini kwamba malengo ya mapato ya ndani, fedha za nje na matumizi, yatafikiwa kama ilivyokadiriwa. Kwa upande wa matumizi, mwelekeo ni kwamba matumizi ya kawaida, hususan matumizi mengineyo *(OC),* hayatafikiwa kutokana na sababu zilizoelezwa awali. Hata hivyo, malengo ya matumizi katika sekta za kipaumbele za kukuza uchumi na kupunguza umaskini, yatafikiwa kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, misingi na shabaha za Bajeti kwa mwaka 2005/2006. Mfumo wa Bajeti ya mwaka 2005/2006 unazingatia utekelezaji wa MKUKUTA. Malengo muhimu ya uchumi ni pamoja na:-

(i) Pato halisi la Taifa linalengwa kukua kwa asilimia 6.9 mwaka huu 2005, asilimia 7.2 mwaka ujao 2006, asilimia 7.6 mwaka 2007 na asilimia 7.9 mwaka 2008.

(ii) Kasi ya upandaji bei itabakia 4 hadi Juni 2005 na baadaye kulingana na viwango vya wastani katika nchi tunazofanya nazo biashara.

(iii) Uwiano kati ya mapato ya Serikali na Pato la Taifa *(revenue/gdp ratio)* utakuwa asilimia 14.3 mwaka 2005/06, asilimia 14.5 mwaka 2006/2007 na asilimia 14.6 mwaka 2007/08 wa fedha.

(iv) Akiba ya fedha za kigeni itatosheleza mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi 7; na mwisho

(v) Ongezeko la ujazi wa fedha (kwa tafsiri pana, M3) litawiana na malengo ya ukuaji wa uchumi na kasi ya upandaji bei nchini.

Mheshimiwa Spika, sera za mapato kwa mwaka 2005/2006, zinalenga kukusanya mapato ya ndani yasiyopungua shilingi 2,066,751 milioni (trilioni 2.067) sawa na asilimia 14.3 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na mapato ya asilimia 13.8 mwaka 2004/2005. Lengo hili la mapato ni ongezeko la asilimia 18.7 kwa mwaka 2005/2006, ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 20.7 linalotarajiwa mwaka tunaomalizia wa fedha 2004/2005. Ili kuendelea kuboresha ukusanyaji, hatua zifuatazo zitatekelezwa:-

(i) Kuimarisha utendaji na usimamizi katika Idara ya Forodha.

(ii) Kurekebisha Muundo wa Mamlaka ya Mapato ili kuboresha zaidi usimamizi wa vianzo vya ndani.

(iii) Kuimarisha Idara ya Walipakodi Wakubwa, ili ihudumie walipakodi wengi zaidi.

(iv) Kufanya marekebisho ya mfumo wa kodi katika maeneo kadhaa ili kurahisisha utekelezaji na ufanisi wa utawala wa kodi.

(v) Kuimarisha ukusanyaji na taarifa za mapato kutoka Wizara na Idara mbalimbali, hasa zile zilizo kwenye utaratibu wa *Retention.*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kukua kwa uchumi na kupanuka kwa wigo wa kodi, mageuzi makubwa yanayoendelea ndani ya Mamlaka ya Mapato chini ya Mpango wake wa Pili wa Miaka Mitano *(Second Corporate Plan)* yamekuwa chanzo muhimu cha kukua kwa mapato ya ndani. Katika mwaka wa 2005/2006, Serikali itaendelea kuiimarisha Idara ya Walipakodi Wakubwa kwa kuboresha mifumo ya utendaji na taaluma na kuhamishia huko makampuni yote ya madini ili kuboresha mawasiliano na kampuni hizo. Aidha, tutaendelea kuboresha usimamizi na utendaji katika Idara ya Forodha kwa kuongeza uwajibikaji, matumizi ya teknolojia na kupunguza mlolongo wa

taratibu ndefu. Katika zoezi hili, Serikali inashirikiana na Kituo cha Ushauri wa Utaalam cha *IMF (East-AFRITAC),* Shirika la Forodha la Kimataifa *(WCO)* na Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo *(UNCTAD). (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza awali, kwa kutumia Mkakati wa Kusimamia Misaada *(Tanzania Assistance Strategy)* na ule wa Madeni *(National Debt Strategy),* Serikali imeendelea kuwa na uhusiano mzuri na nchi wahisani pamoja na Mashirika ya Fedha ya Kimataifa. Misaada na mikopo ya masharti nafuu ya nje itachangia takribani asilimia 41 ya Bajeti ya mwaka ujao wa fedha 2005/2006. Pamoja na nia yetu ya kutaka kujitegemea, bado tunahitaji misaada ya nje ili itusaidie kujenga uwezo wa kujitegemea hatua kwa hatua katika kipindi kijacho, pamoja na kusaidia kutekeleza kwa haraka mikakati ya kufikia malengo ya Maendeleo ya Milenia *(MDGs).* Tutaendelea kushauriana na nchi wafadhili kwa lengo la kuongeza misaada ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, vianzio vingine vya mapato, katika mwaka 2005/2006 Serikali inakusudia kuuza hisa zake zenye thamani ya shilingi 10,420 milioni katika baadhi ya kampuni na mashirika, na kutumia akiba yake katika Benki Kuu ya Tanzania kwa kiasi cha shilingi 259,225 milioni. Papo hapo, Serikali inaangalia upya sera ya kuuza hisa katika mashirika yenye faida na maslahi mengine ya kitaifa, kwa lengo la kutouza hisa zake zote kwenye kila shirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sera za Matumizi, katika mwaka wa fedha wa 2005/2006, Serikali itaendelea kuimarisha nidhamu katika matumizi ya fedha za umma na kuhakiki uwajibikaji. Aidha, utaratibu wa kutumia tulicho nacho *(cash budget)* utaendelea katika mwaka ujao ili kuhakikisha kwamba Serikali inaishi ndani ya uwezo wake. Vile vile, uwezo wa Ukaguzi wa Ndani katika Wizara na Idara za Serikali utaimarishwa kwa kuendelea kutoa mafunzo ili kuwezesha Wakaguzi wa ndani kufuatilia vyema hoja za ukaguzi na kutoa ushauri nasaha kwa maafisa wahasibu. Mafunzo kuhusu taratibu za uhasibu na ukaguzi wa ndani yataendelezwa na kuimarishwa. Serikali inatarajia kupanua mtandao wa malipo kwa kompyuta kwenye Halmashauri zingine 32 za Wilaya katika mwaka ujao wa fedha. Hatua hii inategemewa kuboresha usimamizi wa matumizi katika Halmashauri hizo kwa kuwezesha upatikanaji wa taarifa kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kupanga mgao wa fedha za Bajeti kwa mwaka wa fedha 2005/2006, mambo yafuatavyo yamezingatiwa:-

(i) Asilimia zaidi ya 50 ya Bajeti ya 2005/2006 imetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa vipaumbele vilivyoainishwa katika MKUKUTA ambavyo ni:-

- kukuza uchumi na kuondoa umaskini wa kipato;

- kuimarisha hali za maisha na hifadhi ya jamii; na

- kuimarisha utawala bora na uwajibikaji.

(ii) Aidha, kiasi kikubwa cha fedha kimetengwa kwa ajili ya sekta za huduma za uchumi na huduma za jamii ili kulinda mafanikio yaliyopatikana chini ya Mkakati wa awali wa Kupunguza Umaskini *(PRSP).* Sekta zinazoongoza kwa kutengewa hizo fedha nyingi ni pamoja na Ujenzi, Afya, Elimu, Kilimo na Maji.

(iii) Fedha za kutosha zimetengwa kwa ajili ya gharama zilizobaki za Uchaguzi Mkuu wa mwezi Oktoba 2005. Fedha hizi ikifika Oktoba mwaka huu kwa ajili ya uchaguzi tutakuwa tumetumia shilingi jumla ya shilingi bilioni 88.5 ndizo fedha tutakazokuwa tumetumia kuanzia mwaka wa 2003 kwa ajili ya uchaguzi Mkuu. Kati ya hizo shilingi bilioni 9.9 ndizo zilizotoka kwa wafadhali na nyingine zote takribani bilioni 80 ni kutoka ndani. *(Makofi)*

(iv) Bajeti hii pia imetenga asilimia 4.5 ya bajeti kwa ajili ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. *(Makofi)*

(v) Bajeti hii imetenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa madawa ya kusaidia kurefusha maisha kwa waathirika wa ugonjwa wa UKIMWI pamoja na kupiga vita malaria na kifua kikuu. *(Makofi)*

(vi) Bajeti ya 2005/2006 imetenga fedha za malipo ya mafao ya waliokuwa watumishi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kama alivyokuwa ameahidi Mheshimiwa Rais wakati wa *May Day. (Makofi)*

(vii) Kufuatia uamuzi wa Serikali wa kuongeza idadi ya wanafunzi katika vyuo, Bajeti ya mwaka 2005/2006 imetenga fedha kwa ajili ya mahitaji hayo. Aidha, majadiliano yanaendelea yanayohusisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili kuongeza vyumba vya madarasa, mabweni, maabara na kadhalika katika Vyuo vya Elimu ya Juu. *(Makofi)*

(viii) Serikali imeamua kutenga moja ya nane (1/8) ya Ada ya Ufundi Stadi *(Skills Development Levy)* kwa ajili ya Mfuko wa Elimu *(Tanzania Education Fund)* ili kuongeza kasi ya kupanua miundo mbinu ya elimu nchini. *(Makofi)*

(ix) Bajeti imetenga fedha kwa ajili ya mishahara ya watendaji wote wa Vijiji, ikiwemo ile ambayo haikulipwa kama bado ipo. Hii ni Awamu ya Pili ya mpango huo yaani tutalipa malimbikizo kwa wale ambao bado hawajalipwa licha ya mshahara. Awamu ya kwanza imetekelezwa mwaka huu wa 2004/2005 na ilihusisha watumishi 7,770. *(Makofi)*

(x) Katika Bajeti ya 2005/2006, Mamlaka ya Usafiri wa Anga *(TCAA)* na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege *(TAA)* zitapatiwa mapato yote yatokanayo na Ada ya Viwanja vya Ndege *(Passenger Service Charge),* badala ya asilimia 90 ya sasa, ili kuhimili gharama kubwa za kuendesha viwanja vya ndege. *(Makofi)*

(xi) Juhudi za kuimarisha utawala bora zimezingatiwa. Fedha zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa kupambana na rushwa katika Bajeti za

Wizara zote na pia kupitia bajeti ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, kwa ajili ya kuboresha utendaji wa mfumo wa Mahakama nchini na hasa Mahakama za Mwanzo. *(Makofi)*

(xii) Bajeti hii imetenga asilimia 18 ya mapato ya ndani kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza awali, Serikali inalenga kukusanya mapato ya ndani ya jumla ya shilingi 2,066,751 katika mwaka wa fedha 2005/2006. Kiwango hiki cha mapato ni asilimia 14.3 ya Pato la Taifa. Serikali inategemea pia kupata shilingi 10,424 milioni kutokana na ubinafsishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi, katika mwaka 2005/2006 Serikali imepanga kutumia jumla ya shilingi 4,176,050 milioni. Misaada na Mikopo ya nje (ikijumuisha misamaha ya madeni) itakuwa shilingi 1,724,910 milioni. Kati ya fedha hizi, shilingi 616,165 milioni ni misaada na mikopo ya kusaidia bajeti moja kwa moja na shilingi 93,600 milioni ni misamaha ya madeni, wakati shilingi 1,015,145 milioni ni mikopo na misaada kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kama nilivyoeleza hapo awali, Serikali inakusudia kuuza hatifungani maalum kwenye soko kwa ajili ya miundombinu. Aidha, shilingi 259,225 milioni zitapatikana kwa kupunguza akiba ya Serikali katika Benki Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza jitihada za kuboresha mfumo wa kodi na taratibu za ukusanyaji mapato, Serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika maeneo yafuatayo:-

(a) Sheria ya Kodi ya Mapato;

(b) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT);*

(c) Sheria ya Ushuru wa Forodha;
(d) Ada ya leseni za magari;

(e) Ada ya Leseni za Usafirishaji;

(f) Sheria ya Ushuru wa Stempu; na

(g) Sheria ya Mfuko wa Elimu.

Mheshimiwa Spika, inapendekezwa kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 ili kuongeza kiwango cha chini cha mapato ya ajira yasiyotozwa kodi kutoka shilingi 60,000 kwa mwezi hadi shilingi 80,000 kwa mwezi. Hii ni katika kuitikia mwito wa wafanyakazi kwamba walikuwa wanaumia na huu ni mwanzo. Ningependa kusema kwa sababu ya hali halisi, lakini la msingi ni kwamba Serikali imesikia. Hatua hii ina lengo la kuwaondoa kwenye wigo wa kodi wafanyakazi wa kipato cha chini na kutoa unafuu wa kodi kwa wafanyakazi hao kama njia ya

kutekeleza Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini ni mkakati wa (MKUKUTA). Viwango vya sasa na vinavyopendekezwa vimeonyeshwa katika Jedwali Namba 1. Viwango vya ukokotoaji wa kodi hiyo vimebaki kama vilivyokuwa kwa ngazi mbalimbali za mishahara, yaani asilimia 18.5, 20, 25 na 30.

Mheshimiwa Spika, marekebisho haya yatapunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shillingi 27,970 milioni. Hata hivyo, nyongeza ya mishahara ya watumishi pamoja na ufanisi katika usimamizi wa kodi vinatarajiwa kuongeza mapato na hivyo kupunguza pengo hadi shilingi 1,822 milioni.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* inapendekezwa kufanya marekebisho yafuatayo katika eneo hili la Sheria ya Kodi la Ongezeko la Thamani yaani *VAT*:-

(i) Kufanya marekebisho katika Jedwali la Tatu la Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ili kuingiza kwenye msamaha huo vipuri vya treni na vifaa vingine vinavyotumika katika treini. Marekebisho hayo yatasaidia kupunguza gharama za usafirishaji na kusaidia Mashirika ya Reli ya *TRC* na *TAZARA* kumudu gharama za matengenezo. *(Makofi)*

(ii) Kufanya marekebisho katika Jedwali la Pili la Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ili kuingiza kwenye msamaha huo mafuta ya ndege kwa wenye ndege za kibiashara au huduma za jamii za hapa nchini. Hatua hii inalenga kuwawezesha wenye ndege hizo hapa nchini kuhimili ongezeko kubwa la gharama za kuendeshea ndege, hasa baada ya balaa la Septemba 11 na ongezeko la sasa la bei ya mafuta ya ndege. Hatua hii italinda utalii na ndege zinazohudumia wagonjwa, kilimo, hifadhi, viongozi, Polisi, Jeshi na kadhalika. *(Makofi)*

(iii) Kufanya marekebisho katika Jedwali la Tatu la Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ili kuingiza kwenye msamaha wa *VAT* magari yanayotumika kutoa huduma za afya yaani *Mobile Health Clinics* ili kuvutia huduma hizo katika maeneo yasiyo na vituo vya afya au zahanati. *(Makofi)*

(iv) Kufanya marekebisho katika Jedwali la Tatu la Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kuondoa kifungu cha sasa kinachotoa msamaha wa kodi kwa shughuli za uchimbaji madini kwa vile msamaha kama huo umetolewa kwenye vifungu vingine vya sheria hiyo. *(Makofi)*

Hatua hizi katika kodi ya *VAT* kwa ujumla zitapunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi 2,685 milioni zitapunguza mapato.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, inapendekezwa kufanya marekebisho yafuatayo katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa:-

(a) Mafuta ya Ndege, inapendekezwa kutoa msamaha wa ushuru wa bidhaa kwenye mafuta ya ndege *(Jet A-1)* ili kuwepo usawa katika ushindani kwa faida ya kampuni za ndege za hapa nchini, *level play field* wanaita.

(b) Viwango vya Ushuru wa Bidhaa, inapendekezwa kurekebisha viwango vya Ushuru wa Bidhaa kwa asilimia tano tu, sawa na takriban mfumuko wa bei, kwa bidhaa zifuatazo:-

(i) Vinywaji baridi kutoka shilingi 39.4 kwa lita hadi shilingi 41.5 kwa lita;

(ii) Bia kutoka shilingi 243 kwa lita hadi shilingi 256 kwa lita;

(iii) Mvinyo uliotengenezwa kwa zabibu inayozalishwa nje ya nchi kwa kiwango kinachozidi asilimia 25, kutoka shilingi 780 kwa lita hadi shilingi 820 kwa lita;
(iv) Vinywaji vikali kutoka shilingi 1,158 kwa lita hadi shilingi 1,216 kwa lita;

(v) Kurekebisha mfumo wa kutoza Ushuru wa Bidhaa kwenye sigara ili kutumia kigezo cha kuwa na kichungi *(filter)* badala ya urefu wa sigara pamoja na kurekebisha viwango vya ushuru wa bidhaa kama ifuatavyo:-

(a) Sigara zisizo na kichungi na zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75, kutoka shilingi 3,970 hadi shilingi 4,170 kwa sigara elfu moja; haya ni mambo ya mwaka wa kupunguza uvutaji wa sigara. *(Makofi)*

(b) Sigara zenye kichungi na zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75, kutoka shilingi 9,367 hadi shilingi 9,840 kwa sigara elfu moja. *(Makofi)*

(c) Sigara nyingine zenye sifa tofauti na (a) na (b) kutoka shilingi 17,017 hadi shilingi 17,870 kwa sigara elfu moja. *(Makofi)*

(d) Tumbaku ambayo iko tayari kutengeneza sigara *(cut filler)* kutoka shilingi 8,593 hadi shilingi 9,025 kwa kilo;

(e) Ushuru wa Bidhaa kwa *Cigar* unabaki kuwa asilimia 30. *(Makofi)*

Marekebisho haya ya ushuru wa bidhaa kwa pamoja yanatarajiwa kuipatia Serikali mapato mapya ya kiasi cha shilingi 4,418.6 milioni yaani shilingi bilioni 4.418.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ada ya Leseni za Magari na Usafirishaji zinazokusanywa na Mamlaka mbalimbali, katika eneo hili, inapendekezwa kufanya marekebisho ya viwango vya baadhi ya ada zinazotozwa na vyombo mbalimbali. Lengo ni kuondoa kero, kuboresha mazingira ya biashara na kufidia gharama za usajili wa magari.

(i) Kufuta ada za leseni za usafirishaji zinazotozwa na mamlaka mbalimbali za leseni za usafirishaji, kwa magari yasiyochukua abiria ikiwa ni pamoja na *pick-ups* na magari makubwa ya mizigo. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Rudia!

**WAZIRI WA FEDHA:** Nirudie! Kufuta ada za leseni za usafirishaji zinazotozwa na mamlaka mbalimbali za leseni za usafirishaji, kwa magari yasiyochukua abiria, ikiwa ni pamoja na *pick-ups* na magari makubwa yaani malori ya mizigo. Haya ni mambo ya malori na *pick-ups.*

(ii) Asilimia 20 ya ada.

**WABUNGE FULANI:** Ahaa!!

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, vitabu walivyonavyo Wabunge vinasema asilimia 10, ndiyo maana unasikia wanashangaa.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, asilimia 10, ahaa hapana. Nitasoma yaliyo kwenye kitabu changu. Halafu tutaelewana mbele ya safari. *(Kicheko)*

Hatua ya pili, asilimia 20 ya ada ya huduma kwa abiria wa ndege *(Service Charge)* ambayo inaingia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali sasa itapelekwa kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. *(Makofi)*

(iii) Kuongeza kiwango cha Ada ya Gari kutoka shilingi 10,000.0 hadi shilingi 20,000.0 kwa gari kwa mwaka. Hatua hizi kwa pamoja zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi 1,125 milioni.

Mheshimiwa Spika, inapendekezwa kupunguza kiwango cha ushuru wa stempu kutoka asilimia nne (4%) hadi asilimia moja (1%) ya thamani ya mali husika kwenye maeneo yafuatayo:-

(a) Kubadilishana mali kitu wanachoita *(exchange of property);*

(b) Hati ya Mauzo *(bill of sale);*

(c) Cheti cha mauziano *(certificate of sale);*

(d) Hati ya Zawadi *(instrument of gift);*

(e) Uhamisho wa mali ya kukodi *(Transfer of lease by way of assignment);*

(f) *Instrument of partition;*

(g) *Instrument of release;* na

(h) *Instrument of settlement.* Kama utakavyoviona Mheshimiwa Spika, bado tunatafuta Kiswahili cha mambo haya matatu hayo.

Mheshimiwa Spika, inapendekezwa pia kupunguza kiwango cha Ushuru wa Stempu kwenye utambuzi wa madeni *(acknowledgement of debt)* kutoka asilimia 4 na kuwa shilingi 500 tu. Hatua hizi zitapunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shillingi 1,996 milioni.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mfuko wa Elimu, sambamba na uamuzi wa Serikali wa kuupatia Mfuko wa Elimu moja ya nane (1/8) ya mapato yanayotokana na Ada ya Ufundi Stadi, inapendekezwa kufanya marekebisho katika Sheria ya Mfuko wa Elimu ya mwaka 2001 ili kufuta vifungu vinavyotoa msamaha wa Kodi ya Mapato, *VAT* na Ushuru wa Forodha kwa wanaochangia Mfuko huo ili kufuta vifungu vinavyotoa msamaha wa kodi ya mapato *VAT* na Ushuru wa Forodha kwa wanaochangia mfuko huo.

Hata hivyo, wachangiaji wataendelea kupata punguzo la kodi kwa mujibu wa kifungu cha 16 (1) (b) cha Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004. Kwa vingine hatujafanya lolote kubwa, hatua hii haiongezi wala kupunguza mapato ya Serikali. Inafanya utawala wa kodi hii kuwa nzuri zaidi tu basi.

Marekebisho katika baadhi ya Sheria nyingine za Kodi, inapendekezwa kufanya marekebisho sheria mbalimbali za fedha na kodi ili ziendane na wakati na kurahisisha utekelezaji wake. Hatua hii haina athari kwa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, inapendekezwa kufuta Ada ya Leseni ya Ukazi *(License to reside in a forest reserve)* na Ada ya Leseni ya Kulima kwenye msitu wa Serikali. Hii leseni unapotakiwa kuishi pale siyo kama hautakiwi uende pale kwa kisingizio kwamba Sheria imefutwa hapana. Unapotakiwa na Bwana Misitu kuishi mahali usilipe leseni ya ukaazi ndiyo maana yake. Wala leseni ya kulima kwenye msitu unapokaa pale ukalima kidogo usitakiwe kulipa leseni ya kulima yaani kama Nyarubanja, kama aina ya Nyarubanja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, au kampuni, iwe ni kampuni au msitu wa Serikali, wanaotoza wananchi wanaoruhusiwa kuishi katika misitu ya hifadhi ili kuondoa kero kwa wananchi. Hii ni kero tu.

Aidha, inapendekezwa kwamba leseni za kuendesha biashara katika misitu hiyo, leseni za kuendesha biashara siyo za kukata miti, za kuendesha biashara ya maduka na mambo ya namna ile, zikatwe mara moja tu kama ilivyokwisharekebishwa mwaka jana kwa biashara nyinginezo. Hatua hii haina athari yoyote kwa mapato ya Serikali lakini inaondoa kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, tangu tulipoanza kutekeleza Itifaki ya Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwezi Januari mwaka huu, tumepokea mapendekezo ya marekebisho ya viwango vya ushuru wa pamoja wa Forodha *(EAC Common External Tariff)* kutoka kwa wadau mbalimbali kupitia kamati maalumu ya kurekebisha mfumo wa

kodi nchini. Serikali za Kenya na Uganda pia zilipokea mapendekezo kutoka kwa wadau wao.

Mapendekezo ya Tanzania pamoja na yale ya kutoka Kenya na Uganda yalijadiliwa katika kikao cha Mawaziri wa Fedha wa Nchi Wanachama wa Jumuiya kilichofanyika Arusha tarehe 14 Mei, 2005. Mapendekezo hayo ya Mawaziri wa Fedha yatawasilishwa kwenye kikao cha Kisekta cha Mawaziri wa Biashara, Fedha na Uwekezaji wa Nchi Wanachama wa Jumuiya, kitakachofanyika tarehe 20 Juni 2005, kama ilivyoagizwa na kikao cha Wakuu wa Nchi hizo kilichofanyika Dar es Salaam tarehe 29 - 30 Mei, 2005. Marekebisho yatakayoidhinishwa yatatekelezwa pamoja na hatua nilizozielezea katika Hotuba hii, baada ya uamuzi wa kawaida wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi za kodi mpya na zile zitakazo idhinishwa na kikao cha Mawaziri wa Jumuiya ya Afrika Mashariki cha tarehe 20 Juni, 2005 zitaanza kutumika tarehe 1 Julai, 2005 isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo.

Marekebisho yanayopendekezwa ni kama ifuatavyo:-

(i) Kodi ya Mapato inayotokana na ajira ni (1,822) hasara;

(ii) Hatua ya Ushuru wa Stempu inaleta hasara ya shilingi (1,996);

(iii) Hatua ya Ongezeko la Thamani ni hasara kwa Serikali ya shilingi (2,685);

(iv) Hatua ya Ushuru wa Bidhaa inaiIetea Serikali mapato faida ya shilingi 4,419;

(v) Ada za Leseni zinaiIetea Serikali mapato ya shilingi 2,084. Jumla ni sifuri. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mfumo wa Bajeti niliouelezea hapo juu, sura ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2005/2006 inakuwa kama ilivyo kwenye jedwali namba 2.

Mheshimiwa Spika, kwa muhtasari, Bajeti ya mwaka 2005/2006 itagharimu shilingi trilioni 4, bilioni 176, milioni 50 (4,176,050 milioni).

(a) Mapato ya ndani kutokana na kodi, yasiyo ya kodi na mapya yanategemewa kufikia shilingi trilioni 2, bilioni 66 milioni 752 (2,066,752 milioni).

(b) Mapato kutokana na misaada na mikopo, akiba toka Benki Kuu ya Tanzania, mauzo ya hisa za mashirika, na mikopo ya ndani isiyo ya kibenki yanatarajiwa kufikia shilingi trilioni 2, bilioni 109, milioni 298 (2,109,298 milioni).

Kwa upande wa matumizi ya kawaida, Serikali inatarajia yatafika shilingi trilioni 2, bilioni 790, milioni 867 (2,790,867 milioni). Gharama hizo ni kwa ajili ya Deni la

Taifa, Wizara, Mikoa, Halmashauri, mishahara ya watumishi katika Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Taasisi, pensheni, na dharura.

Matumizi ya maendeleo yatatokana na fedha za ndani shilingi bilioni 370 na za nje shilingi trilioni moja, bilioni 15 milioni 145 (1,015,145 milioni), jumla trilioni moja, bilioni 385, milioni 183 (1,385,183 milioni).

Jumla ya Mapato na Matumizi inawiana, yaani shilingi trilioni 4, bilioni 176, milioni 50 (4,176,050 milioni).

Mheshimiwa Spika, mwisho kazi iliyofanyika katika kipindi hiki cha Awamu ya Tatu ni kubwa na Watanzania wote tunayo haki ya kujivunia na kujipongeza. Lakini naamini tutakuwa wachoyo wa shukrani kama hatutatambua mchango mkubwa na wa kipekee wa Jemadari wetu katika vita hii, ambaye ni Mheshimiwa Benjamini William Mkapa, ambaye kama tunavyofahamu ni Rais wetu na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

. Ni Rais wa nchi na Mwenyekiti wa Chama chetu cha Mapinduzi. Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa amekuwa Kiongozi asiyeyumbishwa katika kulinda maslahi ya Taifa wakati wa kutekeleza mageuzi yaliyotuletea mapinduzi tunayojivunia hapa leo. Hakuyumba wakati baadhi yetu tulipokuwa tukipiga kelele za ukapa, ukata, kuuza nchi na kadhalika. Amedhihirisha uelewa mkubwa wa uchumi wetu na wa duniani, ameonyesha ubunifu wa hali ya juu sana katika kupanga sera na mikakati mbalimbali iliyozaa matunda haya, na amekuwa msimamizi hodari wa utekelezaji na ufuatiliaji wa mikakati iliyoamuliwa. Msimamizi hodari wa ufuatiliaji. Mimi ni shahidi.

Aidha, ushiriki wake katika majukumu ya ndani na hata ya Kimataifa hata alipokuwa mgonjwa, umesaidia sana kuijengea nchi yetu heshima na kuvutia wawekezaji na wahisani. Nchi yetu imekuwa na bahati kubwa kumpata Mheshimiwa Benjamin Mkapa kama kiongozi wetu Mkuu wakati huo na katika kipindi hiki muhimu kwa mustakabali wa Taifa letu. *(Makofi)*

Ni imani yangu kuwa endapo dalili zinazojitokeza kuashiria kuwa Serikali ijayo ya Chama cha Mapinduzi itafuata nyayo za Rais Benjamin Mkapa, zitatimia, matumaini ya wananchi ya kuboresha zaidi uchumi na kuutokomeza umaskini kwa nguvu mpya, ari mpya na kasi mpya, nasema...

**WABUNGE FULANI:** Rudia, rudia!!!

**WAZIRI WA FEDHA:** Ni imani yangu kuwa endapo dalili zinazojitokeza kuashiria kuwa Serikali ijayo ya Chama Cha Mapinduzi itafuata nyayo za Rais Benjamin Mkapa, zitatimia, matumaini ya wananchi ya kuboresha zaidi uchumi na kuutokomeza umaskini, kwa nguvu mpya, ari mpya na kasi mpya, yatafanyika Tanzania, yataifanya Tanzania izidi kumeremeta na kupaa. *(Makofi)*

Binafsi naona fahari kubwa na namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniweka katika timu inayojiandaa kuipisha timu mpya Serikalini baada ya kufunga magoli mengi ilipokuwa uwanjani. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya mwaka 2005/2006 imeandaliwa kuwa daraja la kuendeleza juhudi za Serikali katika:-

(i) Kuhitimisha utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2000 na kuanza Ilani ya mwaka 2005 bila kuzubaa zubaa. *(Makofi)*

(ii) Kuweka misingi ya utekelezaji wa sera za Chama Tawala chini ya Serikali ya Awamu ya Nne. *(Makofi)*

(iii) Kuendelea kuhimiza utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa hadi 2025. *(Makofi)*

(iv) Kuanza kutekeleza Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania - MKUKUTA. *(Makofi)*

(v) Kutekeleza Sera za Kijumla za Kiuchumi kwa mwaka 2005/2006. *(Makofi)*

Hii ni sawa na kusema jiko limeshaandaa vyakula vyote kazi iliyobaki ni kupakua.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa malengo na mikakati niliyoitaja hapo juu inategemea juhudi za dhati za kila Mtanzania, kila mzalendo na kila mwenye nia njema na Taifa letu, ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na huduma za jamii. Lengo letu kubwa ni kuhakikisha umaskini unapungua haraka, hatua kwa hatua. Kama nilivyoeleza hapo awali, uchumi wetu unaendelea kukua kwa kiwango cha kuridhisha.

Hata hivyo, kwa kasi ya ongezeko la watu la takriban asilimia 3 kwa mwaka, itachukua si chini ya miaka 20 kuongeza maradufu pato la wastani la wananchi *(income per capita)* itachukua si chini ya miaka 20 kuongeza maradufu pato la wastani la mwananchi tukiweza kufikia kasi ya kukua kwa uchumi ya asilimia 8 kwa mwaka. Tusipofikia kukua kwa uchumi kwa asilimia 8 kwa mwaka, miaka 20 hatuwezi kuongeza maradufu pato la mwananchi wa kawaida, *this is very threatening news,* inatisha, tukizingatia kwamba pato jipya la wastani bado litakuwa chini ya Dola 2 za Kimarekani kwa siku, ni dhahiri kwamba tutakuwa bado hatujapiga hatua kubwa, hata tukipata mafanikio hayo bado. Kwa hiyo, tunahitaji kuwa wabunifu zaidi na pia kung'ang'ania kusukuma maeneo muhimu katika uchumi, kung'ang'ania kusukuma maeneo muhimu katika uchumi kung'ang'ania ili kupata njia mpya za kuongeza kasi ya kukua kwa uchumi na kufikia zaidi ya asilimia 10 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii inapendekeza kuanza kuchukua hatua katika eneo la miundombinu ya aina aina ambayo imeonekana kuwa ni kikwazo kikubwa kwa juhudi zetu za kukuza uchumi. Katika Awamu inayokuja, mikakati zaidi inahitajika ili kuimarisha na kuendeleza changamoto hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja ya Waziri wa Fedha imetolewa na imeungwa mkono. Kwa taratibu zetu hoja zote mbili iliyotolewa asubuhi na hii ya mchana zitajadiliwa kuanzia kesho kutwa tarehe 10 Juni, 2005. Hadi sasa Waheshimiwa Wabunge waliokwisha kujiandikisha wakitaka kupewa nafasi ya kutoa mchango ni 63.

Waheshimiwa Wabunge, hapo ndiyo tumefikia mwisho wa Kikao cha leo. Kwa hiyo, sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 11.25 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi Tarehe 09 Juni, 2005 saa tatu asubuhi)*